# Nipashe

Jumatatu Machi 30, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580192

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Jiko la mkaa lilivyoua familia ikiwa imelala usiku wa manane

UKURASA 4




UKURASA 13

TISHIO LA CORONA

# KKKT yaja na hatua za ziada

• **Ni** masuala ya ibada, AICT yabadili utaratibu Pasaka, Mara yahitaji mil. 700/-, wanahabari waonywa... *Uk. 2,3,10*




### BAA LA CORONA

**TAARIFA za Shirika la Afya Duniani (WHO), zimeonyesha kuwa hadi jana Machi 29, watu waliothibitika kupata maambukizi ya virusi vya corona (Covid-19) duniani ni 575,444, idadi ya vifo ni 26,654 na nchi, maeneo yaliyoathirika na virusi hivyo ni 202.**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## Washukiwa wa corona kuhudumiwa tiba Kibaha

UKURASA 2




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa tatu kushoto), akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wa nne kushoto) katika hafla iliyofanyika Ofisi ya Waziri Mkuu jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa Benki ya NMB, Alfred Shao na kulia ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. **Habari uk.3. PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Mambo manane ya Zitto kwa JPM kuhusu corona

UKURASA 2


**MICHEZO** **EYMAEL AMTAJA LUSAJO YANGA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# KKKT yaja na hatua za ziada

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), limesema wakati wowote kuanzia sasa, litachukua hatua za ziada katika kukabiliana na kasi ya maambukizi ya homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa kanisa hilo, Askofu Dk. Frederick Shoo, jana wakati akihubiri katika ibada maalum ya kumsimika Mchungaji Biniel Mallyo, kuwa Mkuu wa Jimbo la Hai la Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT.

Mchungaji Mallyo anabeba mikoba hiyo, baada ya mtangulizi wake, Mch. Aminirabi Swai, kufariki dunia Julai mwaka jana.

"Ndugu zangu katika kukabiliana na janga hili la ugonjwa wa corona, huenda tukachukua hatua za ziada katika taratibu zetu za ibada, ingawa hatutaacha kumwabudu Mungu.

"Pamoja na tahadhari zote, hatutaacha kumlilia bwana ili atuepushe na janga hili na kutuponya. Amesema niite nami nitaitika. Tutamlilia nani zaidi ya Mungu ambaye ni kimbilio letu."

Akihubiri katika Usharika wa Hai Mjini, Askofu Dk. Shoo ambaye ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, alisema huu ni wakati wa kumkaribia Mungu, kwa kuwa inaonekana kwa nguvu zetu na akili zetu za kibinadamu, hatuwezi zaidi ya kimkimbilia yeye.

Aliwatia matumaini Watanzania, akieleza kuwa ugonjwa huo wa corona utapita maana Mungu amesema atawalinda dhidi ya mauti na magonjwa.

Pamoja na mambo mengine, Askofu Dk. Shoo aliwasihi Wakristo nchini kuwaombea watumishi wa sekta ya afya wanaotoa huduma dhidi ya waliothibitika kuugua ugonjwa huo.

Alitangaza maombi maalum nchi nzima, akitaka kuomba Mungu aliepushe taifa na ongezeko la wagonjwa wa corona.

Kabla ya kuanza kwa ibada hiyo, timu ya madaktari na maofisa wa idara ya afya Wilaya ya Hai, ikiongozwa na Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Irene Haule, iliwapima waumini zaidi ya 1,000 kiwango cha joto kwa kutumia vifaa maalum vya 'themoscan'.




Muuguzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kongwa, Daniel Mbogo (kulia), akimpa ushauri wa kiafya Lidya Kiza, kwenye mmoja ya mikutano ya kijamii wilayani hapo juzi, hospitali hiyo imekuwa na utaratibu wa kutoa huduma za kiafya kwenye mikusanyiko ya kijamii. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mambo manane ya Zitto kwa JPM corona

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ametoa mapendekezo manane kupitia barua aliyomwandikia Rais John Magufuli, kuhusu nini kifanyike katika kuzuia maambukizi mapya ya ugonjwa wa corona.

Zitto ambaye ni Mbunge wa Kigoma Mjini, kwenye barua hiyo alitoa pia ushauri juu ya namna nzuri ya udhibiti wa maambukizi ya ugonjwa huo, ambao umekuwa tishio katika nchi nyingi duniani.

Kwanza, Zitto alipendekeza kuwapo kwa umoja wa kitaifa ambao utawaweka Watanzania pamoja kwa vitendo hali itakayofanikisha kupambana na ugonjwa huo.

"Hakuna wakati nchi yetu inahitaji umoja kama wakati huu. Wewe kama mkuu wa nchi una wajibu mkubwa wa kuwaweka Watanzania pamoja kwa vitendo. Tukiwa wamoja tutaweza kupambana na corona na kushinda pamoja na ikibidi kushindwa tushindwe pamoja," alisema Zitto na kuongeza:

"Corona haitambui itikadi zetu za vyama, dini zetu wala makabila yetu. Corona inaua mashekhe na makasisi, wanasiasa na wananchi wa kawaida, wanadiplomasia na wanamichezo na mbaya zaidi inaua hata wataalamu wa afya kama madaktari na manesi. Nakusihi sana, uunganisha nchi yetu sasa bila kuchelewa," alisema Zitto.

Pili, Zitto alipendekeza wataalamu kupewa nafasi katika kuongoza mapambano na kwamba viongozi kuepuka kutoa maeneo ya jumla.

"Ni muhimu sana sisi viongozi kuepuka kutoa maneno ya jumla ambayo yanawapa wananchi wetu matumaini hewa, hivyo kusababisha hatari zaidi. "Tutoe nafasi kwa wataalamu wa afya kutuongoza katika mapambano haya ya kudhibiti corona. Ni lazima sasa, maneno tunayoyasema kwa umma na maamuzi tunayoyachukua katika kudhibiti mlipuko huu yazingatie ushauri wa wataalamu badala ya imani zetu au fikra zetu," alisema Zitto.

Tatu, alipendekeza serikali kuweka nguvu kubwa kwenye kupima wananchi ili kuwatambua wenye maambukizi, kuwatenga wasiambukize wengine, kuwatibu na kuwafutilia maendeleo yao.

Zitto alisema kazi ya upimaji iwe kampeni endelevu na kwamba serikali itumie vipimo ilivyosaidiwa sambamba na kutumia fedha za dharura ambazo Bunge lilizipitisha kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 kununua vipimo vingi zaidi ili kupima wananchi.

Nne, Zitto alipendekeza kuwapo na uwazi wa takwimu za maambukizi mapya, wagonjwa mahututi na vifo kwani suala hilo ni muhimu sana katika kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema uwazi umesaidia sana nchi kama Korea ya Kusini, na usiri umeathiri kwa kiwango chake nchi ya China na kwamba nchi isione aibu kuweka wazi idadi ya wagonjwa.

Tano, Zitto alipendekeza kuepukwe maelekezo yanayopinga na kueleza kuwa hatua zichukuliwe kusimamisha vikao vyote vya kiserikali ikiwamo Bunge na Mahakama.

"Serikali ilichukua hatua muafaka kufunga shule na vyuo kote nchini ili kuzuia maambukizi. Hata hivyo, tunatuma ujumbe gani kwa wananchi, na hasa watoto wetu wanapoona wao wamefunga shule, lakini viongozi wanahutubia makumi ya watu hadharani? Wanapata ujumbe gani wanapoona Bunge linaendelea na vikao?" Alisema Zitto.

Sita, alipendekeza mahabusi na wafungwa waachiliwe na warudi nyumbani ama kumalizia vifungo au kusubiri upelelezi wa kesi zao.

Zitto alisema: "Mwendesha Mashtaka wa Serikali aondoe zuio la dhamana kwa kesi zote ambazo zilizuiwa dhamana na zile ambazo hazina dhamana kisheria, lakini upelelezi unaendelea watuhumiwa wasubiri upelelezi wakiwa majumbani mwao ili kupunguza msongamano magerezani.

"Watuhumiwa au wafungwa wenye umri zaidi ya miaka 65 na wagonjwa wenye magonjwa hatarishi kwa corona waachiliwe warudi majumbani mwao ama kumalizia vifungo au kusubiri upelelezi wa kesi zao."

Saba, Zitto alipendekekeza kufungwa kwa mipaka ya nchi kwa muda ili kudhibiti maambukizi, na kwamba kwa kufanya hivyo kutasaidia kuzuia maambukizi zaidi.

"Ni lazima kuzuia msongamano wa watu kwenye huduma za usafiri wa umma kwa kuagiza vyombo vya usafiri vya Jeshi la Wananchi, Polisi na hata watu binafsi kutoa huduma ya usafiri wa umma kwa uangalifu mkubwa," alisema Zitto.

Nane, Zitto alipendekeza kuundwa kwa timu ya wachumi waliobobea waliopo ndani na nje ya serikali watakaofanya uchambuzi wa kina wa hali ya uchumi wa nchi na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua.

# Washukiwa wa corona kuhudumiwa tiba Kibaha

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani imetengwa kwa ajili ya kuwahudumia watu watakaogundulika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Waaziri MMkuu, Kassim Majaliwa, ametembelea eneo hilo na kusema ameridhishwa na maandalizi.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wilayani Kibaha.

Alisema serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na corona, ambapo kwa sasa watu wote wanaoingia nchini kupitia viwanja vya ndege, vituo vya mabasi na bandari lazima wapimwe na wakigundulika wanamaambukizi wanawekwa kwenye maeneo maalumu kwa muda wa siku 14.

"Tunazingatia sana wale wanaotoka kwenye nchi ambazo zimeathirika sana wakiingia Tanzania tunawazuia kwanza, tunawapima na tunafuatilia historia yake anatoka wapi na tunaangalia katika siku 14 amepita kwenye nchi zipi."

Alisema wanawekwa kwenye maeneo maalumu ili kuwapima kila siku na kujiridhika kama hawana maambukizi kwani mtu anaweza kupimwa leo akaonekana yuko vizuri, lakini ana maambukizi ambayo hayaonekani kwenye vipimo.

Kwa mujibu wa Majaliwa, kama katika kipindi cha siku 14 mtu atabainika hana maambukizi, anaruhusiwa kwenda kujiunga na familia.

Pia alisisitiza wananchi waendelee kufuata maelekezo yaliyotolewa na serikali kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo ikiwamo kuzuia mikusanyiko, na kwa wale wanaosafiri kwenye usafiri wa umma wasibanane kila mtu akae kwenye kiti.

Waziri Mkuu alisema wananchi wanapokwenda kufuata huduma kwenye masoko wahakikishe wanapeana nafasi baina ya mtu mmoja na mwingine na kabla hawajaingia katika maduka wanawe mikono kwa sabuni na maji tiririka ili kujikinga na maambukizi ya corona.

## HABARI KITAIFA

# NMB yaipa serikali mil. 100/- za corona

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetoa msaada wa Sh. milioni 100 kwa serikali kwa ajili ya kusaidia katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi baada ya kukabidhi fedha hizo kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema benki yao ina jukumu la kuiunga mkono serikali katika vita dhidi ya ugonjwa wa virusi vya corona kwa mustakabali wa afya za Watanzania.

"Kama benki, tumeamua kuungana na serikali katika vita dhidi ya ugonjwa huu kwa kutoa msaada wa Sh. milioni 100 zitakazosaidia katika kuudhibiti," alisema Zaipuna.

Aidha, Zaipuna aliwasihi Watanzania na wateja wa benki hiyo kufuata maelekezo yanayotolewa na serikali kuhusiana na namna ya kujikinga, ikiwamo kuwana mikono pamoja na kutosalimiana kwa kushikana mikono.

Kwa upande wake, Waziri Mkuu Majaliwa baada ya kupokea fedha hizo aliushukuru uongozi wa NMB kwa kuungana na serikali katika kupambana na ugonjwa huo.

Majaliwa alisema, "Msaada wa NMB umekuja muda mwafaka wakati tunafanya mkakati wa kupambana na ugonjwa huu," na kuongeza:

"Tulichokipokea leo kutoka taasisi mbalimbali inadhihirisha kuwa wako na sisi katika kipindi hiki kigumu na wamekuja kutuunga mkono katika mapambano na ugonjwa huu, tunawashukuru sana."

Ugonjwa wa corona ulioanzia katika Jiji la Wuhan nchini China hadi sasa umeshaua idadi kubwa ya watu duniani, huku wengine wakiwa wameambukizwa.

Katika nchi za Ulaya kama Italia na Hispania, ugonjwa huo umeendelea kuua idadi kubwa ya watu, hali inayosababisha shughuli za kijamii kusimamishwa na wananchi kujifungia ndani.



Mmoja wa wafanyabiashara wa Soko la Samunge lililopo Kata ya Mjini Kati wilayani Arusha, jana, akijaribu kuzima moto kwenye mabaki ya vibanda vilivyoteketea usiku wa juzi majira ya saa 5:30. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Tarime yajizatiti corona mipakani

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MKOA wa Mara unahitaji Sh. milioni 700 ili kuhimili mapambano ya kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona hususan wilaya zinazopakana na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Mamlaka mkoani hapa imedai kipaumbele kimewekwa katika kuimarisha mbinu za uhamasishaji kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya vijijini na kukagua kama wanatii maagizo ya serikali yaliyotolewa ikiwa ni pamoja na kuepuka misongamano na kunawa mikono mara kwa mara na maji yaliyotiwa dawa au sabuni.

Akizungumza wakati wa ziara ya kamati ya usalama ya mkoa ya kukagua vituo vya kudhibiti maambukizi maeneo ya mpakani wilayani hapa, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, alisema hivi sasa hakuna visa vyovyote vya maambukizi vilivyoripotiwa maeneo hayo.

Alisema tayari wamewasilisha maombi ya dharura Serikali Kuu kuhusu kupewa msaada huo wa dharura wa fedha ili kuhimili mahitaji ya vifaa kinga na udhibiti zikiwamo barakoa na kuongeza vituo vya upimaji.

"Tunahitaji fedha kuendesha zoezi la uhamasishaji kwa wakazi wote wanaoishi katika maeneo ya vijiji vya mpakani na nchi jirani kuepuka kupokea wageni ambao hawapiti katika njia rasmi, wanatakiwa kupitia vipimo kabla ya kuruhusiwa kuvuka kuingia nchini," alisema Malima.

Alisema hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wafanyabiashara au waendesha pikipiki 'Bodaboda' ambao watatumia mwanya wa kujinufaisha kifedha kipindi hiki cha udhibiti kwa kuvusha watu kupitia njia za panya ambao hawana vibali vya kusafiri.

"Mara nyingi uzoefu unaonyesha baadhi ya wananchi ambao sio wazalendo wanatumia mwanya wa kujinufaisha kiuchumi kupitia majanga mbalimbali ikiwamo ugonjwa wa corona, tabia ambayo inapaswa kukoma mara moja," alisema.

Katika hatua nyingine Malima amewataka watendaji wote wa serikali mkoani hapa, kusimamia kikamilifu maagizo yaliyotolewa na serikali katika maeneo yao kwa kuhakikisha wananchi wanatii na kutekeleza kanuni za kiafya kujikinga na maambukizi.

"Wakuu wa wilaya, wakurugenzi, maofisa tarafa, kata na vijiji wahakikishe wafanyabiashara wote wakiwamo wamiliki wa hoteli, baa na migahawa wanaweka vifaa vya kunawia mikono na sabuni pamoja na magari yote ya abiria na binafsi hayazidishi abiria," alisema.

# Waandishi watakiwa kujilinda, kuripoti usahihi Covid-19

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAANDISHI wa habari nchini wameshauriwa kuwa makini wakati wanaporipoti habari za ugonjwa wa corona na kujihakikishia usalama wao kwa kupeleka elimu na taarifa sahihi kwa jamii.

Ushauri huo ulitolewa na mtaalamu wa masuala ya mawasiliano kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), Dk. Joyce Bazira, mjini hapa.

Tamwa walifika mjini hapa kwa lengo la kuwapatia waandishi wa mikoa ya Lindi na Mtwara, elimu ya kuripoti taarifa inayohusu ugonjwa wa corona ambao tayari umeshapoteza idadi kubwa ya watu duniani.

Hata hivyo, mafunzo hayo hayakufanyika kutokana na vyombo vya dola kuzuia mikusanyiko ya watu kufuatia tishio la ugonjwa huo.

Akizungumza na gazeti hili, Dk. Bazira alisema ugonjwa wa corona unaosababishwa na virusi vya Covid-19 haukuanzia hapa nchini, kwa sababu hiyo wengi wanajifunza na kutafuta taarifa zinazohusu ugonjwa huo kwa njia mbalimbali, kama vile mitandao, vyombo vya habari vya nje, vikiwamo vya nchini ugonjwa ulikoanzia.

Dk. Bazira alisema hali hiyo imesababisha kuwapo kwa taarifa nyingi ambazo kati ya hizo nyingine sio zenye usahihi bali zinapotosha jamii. "Ninachowaomba ndugu zangu waandishi muwe makini na hizi taarifa hasa za mitandaoni," alisisitiza Dk. Bazira.

Alisema ili waandishi wa habari Watanzania waweze kuelimisha kwa usahihi kuhusu ugonjwa huo, ni lazima wao wenyewe kwanza wawe na elimu ya kutosha kuhusu ugonjwa huo, asili yake, jinsi unavyomwathiri binadamu, namna unavyoambukiza na hatua za kujikinga.

Alisema iwapo waandishi wa habari hawatakuwa na elimu sahihi, itakuwa si jambo jepesi kuwapatia jamii elimu sahihi, hivyo vita dhidi ya ugonjwa huo itakuwa na upungufu.

Dk. Bazira alisema kundi la waandishi lipo kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa iwapo halitakuwa na elimu ya kutosha na sahihi ya namna ya kujikinga na hasa wanapotekeleza majukumu yao ya kazi.

Alisema kuwa pamoja na serikali kukemea kuhusu mikusanyiko ya watu, lakini yapo maeneo mengi bado makundi na mikusanyiko ipo, na kuitaja baadhi kuwa ni pamoja na vyombo vya usafiri.

"Maeneo kama haya mwandishi angependa kutekeleza majukumu yake, asipokuwa mwangalifu anaweza kujikuta anakuwa mmoja wa waathirika kwa kupata ugonjwa wa corona," alisema.

Dk. Bazira alisema pamoja na serikali kuviomba vyombo vya habari na waandishi wasaidie kutoa elimu inayohusu ugonjwa huo, ukweli ni kwamba waandishi wenyewe wangepaswa kuelimishwa pia ikizingatiwa mazingira ya sasa watu wengi kujiingiza kwenye fani hiyo.


UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**INVITATION TO BID (ITB)**

**ESTABLISHMENT OF LOCAL FRAME AGREEMENTS FOR SUPPLY AND DELIVERY OF ASSORTED NON-FOOD ITEMS**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified suppliers and manufacturers to submit firm offers for Establishment of multiple Frame Agreements for the supply and delivery of any or all of the below listed Non-Food Items.

**2. Requirement:**

| TENDER REFERENCE NUMBER | TENDER ITEM DESCRIPTION |
|---|---|
| ITB/2020/SUP/013 | Fleece Blankets |
| ITB/2020/SUP/014 | Wrappers (Khanga) |
| ITB/2020/SUP/018 | Multi-purpose Soap Bars |

**3. Eligibility:**

Manufacturers, authorized resellers, wholesalers, or traders duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's needs are invited to participate in the bidding process.

The tender documents can be collected from the following UNHCR Offices:

UNHCR Representation Office Tanzania
Plot 1658 Masaki, Rufiji Street
P.O Box 2666 - **Dar es Salaam**

UNHCR Field Office Kasulu
Kimobwa (Mlimani Area)
P.O. Box 332 - **Kasulu, Kigoma**

UNHCR Sub- Office Kibondo
Kabigwa (Near TANESCO)
P.O. Box 49, **Kibondo**

UNHCR Field Unit Mwanza
Mwanza Airport
P.O. Box 2273 – **Mwanza**

215673002

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Deadline for receiving requests for clarification | Tuesday 31st March 2020 at 16.00 hours EAT |
| Deadline for submission of offers | Tuesday 28th April 2020 16.00 hours EAT |

***UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.***

# Wanne familia moja wafa wakiwa wamelala usiku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATU wanne wa familia moja katika kitongoji cha Ngilimba 'B' katika Kijiji cha Ngilimba Kata ya Ulowa wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamekufa, kutokana na kuvuta hewa yenye sumu ya carbon monoxide usiku wakiwa wamelala.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, tukio hilo lilitokea juzi saa tisa usiku. Aidha, alisema kuwa sababu za vifo hivyo ni waliacha jiko la mkaa likiwa limewashwa ndani ya nyumba yao, kutokana na baridi iliyosababishwa na mvua kubwa kijijini hapo. Pia Kamanda Magiligimba alisema wanafamilia hao walifunga milango yote na madirisha, hali iliyosababisha kuwapo kwa hewa ndogo ndani ya nyumba yao na kuvuta hewa ya sumu.

"Mvua ilinyesha kubwa huko Ulowa na kusababisha kuwapo kwa baridi...waliwasha jiko la mkaa na wakati wanajiandaa kwenda kulala walifunga madirisha na milango na kusababisha kuwapo kwa hewa chafu yenye sumu ambayo imesababisha kupoteza maisha yao," alisema Magiligimba. Aliwataja waliokufa ni Masanja Emmanuel (35), Mngole Masanja (25), Holo Masanja (5) na Matama Masanja, ambaye umri wake haukufahamika.

Alisema miili ya wanafamilia hao imekabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi baada ya kufanyiwa uchunguzi wa daktari.

Aliwataka wananchi kuacha kufunga milango na madirisha wanapokwenda kulala wala kuacha majiko ya mkaa yakiwa yamewashwa.



Ofisa Afya wa Hospitali ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Nathan Kilumbo, akipima joto la mwili la mmoja wa wananchi waliokwenda kuwaona wagonjwa waliolazwa hospitalini hapo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sita wajeruhiwa na fisi aliyevamia kijiji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATU sita wakazi wa kijiji cha Mwangalanga, Kata ya Samuye wilayani hapa, wamejeruhiwa na fisi wakati wakimshambulia.

Tukio hilo lilitokea Machi 27, saa 10 jioni, katika kijiji cha Mwangalanga wakati fisi huyo alipovamia kijiji hicho na wananchi kumzingira kwa kumpiga na kusababisha watu hao sita kujeruhiwa.

Taarifa iliyotolewa juzi na Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Deborah Magiligimba, ilisema baada ya watu hao kujeruhiwa walikimbizwa hospitali kupatiwa matibabu na hali zao zinaendelea vizuri.

Aliwataja waliojeruhiwa kuwa ni Zengo Jitonja, Nkuba Deteba, Juma Salaganda, Limbu Mihambo, Dutu Mdese, na John Matanda.

"Watu hawa wakati wakiwa wamemzingira fisi huyo na kuanza kumshambulia, aliwang'ata sehemu mbalimbali za miili yao, majeruhi watano walipata majeraha madogo na wemeruhusiwa kutoka hospitali," alisema Magiligimba.

"Majeruhi mmoja Nzengo Jintonja, ambaye alijeruhiwa vibaya kwa kung'atwa mikononi na mdomoni, yeye alikimbizwa na kulazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga na hali yake siyo mbaya sana," aliongeza.

Alisema fisi huyo ameshauawa na wananchi walioendelea kumshambulia kwa kumpiga.

# Agizo la JPM lawafanya kujenga kituo cha afya usiku na mchana

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

UONGOZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, umeanza ujenzi wa usiku na mchana kukamilisha jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya cha Magubike, baada ya agizo la Rais Dk. John Magufuli aliyewataka kufanya hivyo haraka, baada ya kupokea malalamiko ya wananchi kutumia muda na gharama kubwa kufuata huduma za upasuaji maeneo ya mbali.

Ujenzi wa kituo hicho kilichojengwa toka mwaka 1966, unafanywa kwa kuwashirikisha wananchi wanaojitolea nguvu kazi kutokana na umuhimu wa jengo hilo ambalo likikamilika litahudumia zaidi ya wananchi 70,000 wa kata saba zinazopakana na Magubike.

Kata hizo ni pamoja na Mtumbatu, Kiegeya, Maguha, Mamboya, Berega na Kitange na kuhudumia majeruhi wa ajali katika barabara kuu ya Morogoro - Dodoma inayokatiza jirani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, Asajile Mwambambale, alimwahidi Rais Magufuli kuwa wangekamilisha ujenzi huo ndani ya siku 60, toka Machi 16, alipozulu ujenzi wa daraja la Kiegeya lililozolewa na maji na kupokea malalamiko ya wananchi. Alisema siku chache kabla ya muda uliopangwa, Juni 10, wanatarajia jengo hilo litakuwa tayari limekamilika na kusubiri zaidi upatikanaji wa vifaa ili kuanze kutumika.

"Hatukuwa na bajeti kwa ajili ya jengo hili, lakini baada ya Rais kutuelekeza kulikamilisha, tuliitisha kikao cha Baraza la Madiwani cha dharura na kuanza kupunguza huku na kule, tukajibana hadi zikapatikana Sh. milioni 40 tumeshazileta kwenye akaunti ya kata na tunatarajia kutumia zaidi ya Sh. milioni 100 kukamilisha, tumeanza na hatua ya kumwaga jamvi baada ya kupandisha msingi na kujaza mawe," alisema.

Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Sebastian Kamonga, alisema licha ya kukabiliwa na changamoto ya kuwapa rufani wagonjwa wao kwenda maeneo ya mbali kufuata huduma za upasuaji, wanakabiliwa na uchelewaji wa dawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD), na uhaba wa watumishi katika kada mbalimbali.

"Sasa mnaona mawe yamejazwa na jamvi limeshatandikwa, tunaona kama tayari jengo limeshakamilika na wananchi wamejitokeza kwa wingi kujitolea ujenzi," alisema Dk. Kamonga.

Diwani wa Kata ya Magubike, Ernest Chilolo na baadhi ya wananchi Gideon Hosea na Elizabeth Sengoli walimshukuru Rais Magufuli kwa hatua ya haraka kutatua kero hiyo iliyodumu kwa muda mrefu ambayo iliwafanya kufuata huduma za upasuaji maeneo ya mbali na kushindwa kumudu gharama.

Kituo hicho licha ya kupokea wagonjwa mbalimbali, wengi wakisumbuliwa na magonjwa ya malaria, njia ya hewa na kichomi, kimekuwa kikitoa pia huduma za mama na mtoto na kupokea majeruhi wa ajali za barabarani kutokana na kuwa jirani na barabara kuu ya Morogoro -Dodoma.

# Mtaalamu: Dawa zisizothibitishwa kutibu corona hatari kwa afya

**Na Enock Charles**

WANANCHI wametakiwa kuepuka kutumia dawa ambazo hazijathibitishwa na wataalamu au mamlaka kujitibu na ugonjwa wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19) kwa kuwa kufanya hivyo ni hatari kwa afya zao.

Akizungumza na gazeti hili kuhusu dawa ya Chloroquine kudaiwa kutibu ugonjwa wa corona, Mtaalamu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Meshack Chinyuli, alisema wananchi wanapaswa kusikiliza mamlaka husika kwa sababu mara nyingi linapokuja suala la dawa au chanjo huwa kuna protokali yake kuanzia kuifanyia utafiti na hata kuithibitisha dawa kwa ajili ya matumizi pamoja na Rais wa Marekani, Donald Trump kusema inaweza kutibu, lakini lazima ipate kibali kutoka hapa ndani," alisema Dk. Chinyuli.

"Ushauri wangu ni kwamba wananchi wasikilize mamlaka husika kwa sababu mara nyingi linapokuja suala la dawa au chanjo huwa kuna protokali yake kuanzia kuifanyia utafiti na hata kuithibitisha dawa kwa ajili ya matumizi pamoja na Rais wa Marekani, Donald Trump kusema inaweza kutibu, lakini lazima ipate kibali kutoka hapa ndani," alisema Dk. Chinyuli.

"Hata hapa kwetu kutakuwa na mchakato unaoendelea unaofanywa na wataalamu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na sio tu Chloroquine pekee na baadaye kupelekwa katika Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa uthibitisho zaidi," alifafanua.

Hivi karibuni Rais wa Marekani Trump aliwatangazia wananchi wake kuwa dawa aina ya Hydroxychloroquine imeonekana kuleta matumaini baada ya kuleta matokeo mazuri na kuhakikisha kwamba inapatikana kila mahali nchini humo.

Kwa mujibu wa Trump, Idara ya Chakula na Dawa (FDA) ya nchini humo, imeifanyia utafiti dawa hiyo na kuwa anaamini kuwa inaweza kuleta tofauti kubwa duniani katika vita dhidi ya Covid -19 katika mwili.

Hadi sasa Shirika la Afya Duniani (WHO) limeutangaza mlipuko wa virusi vya corona kuwa ni janga la kimataifa, huku mlipuko huo ukiendelea kusambaa katika mataifa mbalimbali duniani na kusababisha vifo na pia hakuna dawa ya moja kwa moja ya tiba au chanjo ya ugonjwa huo iliyotambulishwa na shirika hilo.

Kwa mujibu wa tovuti ya WHO, duniani kuna watu 575,444 walioambukizwa, huku vifo vikiwa ni 26,654 na nchi pamoja na maeneo ya utawala yenye ugonjwa huo ni 201.

Nchi inayoongoza kwa watu wake kuugua ni Italia yenye watu 86,498, Marekani - 85,228, China - 82,239, Uhispania - 64,059, Ujerumani - 48,582, Iran - 35,408, Ufaransa - 32,542, Uingereza - 14,547 na Uswizi - 12,104.



Wakazi wa kijiji cha Buraga, Kata ya Bukumi, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakishiriki ujenzi wa darasa kwa ajili ya shule ya awali (shikizi), katika Kitongoji cha Mwaloni juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mfanyabiashara ajimiminia risasi na kufariki Songea

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MFANYABIASHARA na mkandarasi, mkazi wa Mpambalyoto, Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, Justin Rwendera (64), amekutwa amekufa baada ya kujifyatulia risasi mdomoni na kutokea kwenye sikio la mkono wa kulia.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema tukio hilo lilitokea Machi 29, saa moja asubuhi nyumbani kwake mtaa wa Mpambalyoto.

Alisema kuwa inadaiwa siku ya tukio majira ya saa moja asubuhi, Amida Mnali (47), mkazi wa Bombambili, Songea Mjini, mpishi wa Rwendera na mfanya usafi kwenye nyumba hiyo, aliingia ndani na kumkuta bosi wake akiwa amelala kwenye kochi huku chini kukiwa na bunduki aina ya pisto na damu nyingi zikiwa zimetapakaa. Alisema aliamua kutoa taarifa kwa kuwajulisha ndugu na polisi kuhusu tukio hilo.

Alisema kuwa Machi 28, majira ya saa 11 jioni, Rwendera alirudi nyumbani kwake kutoka kwenye matembezi akiwa amelewa na kukuta kijana wa kaka yake Raurian Bathromeo (43), ambaye ni dereva wa greda linalomilikiwa na marehemu na kumwomba ampatie chakula.

Alisema baada ya kula chakula hicho muda mfupi alitoka kuelekea kwenye zizi la ng'ombe kisha mtoto wa kaka yake aliondoka kwenda nyumbani kwake eneo la Ruvuma.

Kamanda Maigwa alisema polisi walipofika katika eneo la tukio, walikuta bastola ikiwa na risasi saba pamoja na ganda moja la risasi huku mwili wake ukiwa kwenye kochi.

Alisema kuwa bunduki hiyo inashikiliwa na Jeshi la Polisi wakati uchunguzi wa tukio hilo ukiwa unaendelea na hakuna mtu yeyote anayeshikiliwa kuhusiana na tukio hilo, chanzo cha tukio hakijajulikana na uchunguzi wa tukio hilo unaendelea.

# Auawa kwa tuhuma za kuiba mbuzi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKAZI wa Ilembo mkoani Katavi, Omary Sudi (28), amefariki dunia katika hospitali ya mkoa huo alikokuwa akipatiwa matibabu baada ya kushambuliwa kwa kipigo na wananchi wakimtuhumu kuiba mbuzi.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo Kamanda wa Polisi mkoani humo, Benjamin Kuzaga, alisema polisi ilipata taarifa na baada ya kufika eneo la tukio wananchi walikimbia.

Alisema walimwacha mtuhumiwa akiwa na hali mbaya na polisi ilimchukuwa na kumpeleka hospitali na wakati akipatiwa matibabu alifariki dunia.

"Tulipokea taarifa saa tano usiku kuwa maeneo ya Ilembo kuna mtu amepigwa na wananchi baada ya kutuhumiwa kuiba mbuzi wakaamua kujichukulia sheria mkononi," alisema Kuzaga.

Donata Mpandangazi, Mwenyekiti wa Mtaa wa Majengo ambako bibi wa marehemu anaishi, alisema tabia za kijana huyo hazikuwa nzuri kwa kuwa alisumbua kwa wizi katika mtaa huo na baada ya kudhibitiwa na kamati ya ulinzi walihamia kuiba mitaa mingine akiwa na wenzake.

"Taarifa hizi nimezipata na kijana huyu alisumbua sana hapa mtaani akiwa na wenzake, kila wakikamatwa wanatoka wakaanza kuiba mtaa mingine," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya familia bibi wa marehemu alisema alipokea taarifa kuwa Sudi amefariki kwa kupigwa wakisema ameiba.

"Mimi nimemkuza marehemu alikuwa hana tabia ya wizi labda tabia zingine, nilishangaa kuambiwa amejiunga na kikundi cha wizi," alisema bibi wa marehemu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu Ligi Kuu Bara zisikurupuke usajili

**NI** wiki mbili zimepita tangu serikali kutangaza shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo kusimama kwa kipindi cha mwezi mmoja ili kuepuka kasi ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19).

Hatua hiyo iliyochukuliwa na serikali imetokana na kuwapo kwa maambukizi ya virusi hivyo hapa nchini ambavyo vilianzia mji wa Wuhan huko China kabla ya kuenea nchi 199 duniani huku vikiripotiwa kusababisha vifo 31,771 hadi kufikia jana mchana na wagonjwa wakiwa zaidi ya 657, 140.

Aidha, licha ya Tanzania kuripotiwa kuwa na waathirika 13 wa COVID-19, hapajaripotiwa kifo kilichotokana na virusi hivyo wakati huu Italia ikiongoza kwa vifo 10, 023, Hispania (5, 690), China (3, 306), Iran (2, 517) na Ufaransa vifo 2, 314 hadi jana mchana.

Hata hivyo, wakati huu Ligi Kuu Bara ikiwa imesimama kama zilivyo ligi mbalimbali duniani ili kupunguza kasi ya maambukizi ya corona, pilikapilika kubwa za michezo nchini kwa sasa zimehamia kwa viongozi wa klabu kuanza kuwasainisha wachezaji mikataba mipya kwa wale waliomaliza.

Mbali na zoezi hilo ambalo kwetu sisi tunaliona kuwa muhimu, pia tetesi za wachezaji kutakiwa na klabu nyingine kutoka zao za awali ni suala linalotikisa anga za michezo nchini kwa sasa.

Miongoni mwa wachezaji ambao wapo katika mawindo makubwa kwa sasa ni pamoja na beki wa Coastal Union ya Tanga, Bakari Mwamnyeto anayehusishwa na Simba na Yanga. Lakini pia kiungo wa Yanga, Mkongomani Papy Tshishimbi naye anagonga vichwa vya vyombo vya habari nchini akihusishwa na watani zao, Simba. Hatuna shaka na mchakato huo, kwa kuwa tunatambua biashara ni asubuhi jioni ni mahesabu, lakini pia tunazitahadharisha klabu kutokukurupuka katika mchakato mzima wa usajili pasipo kumulika kwanza mashindano yaliyo mbele yao na aina ya wachezaji zinaowasajili kwa sasa.

Tunayasema hayo hasa tukikumbuka namna Yanga ilivyoingia sokoni kwa pupa katika dirisha kubwa lililopita na kufanya usajili uliowagharimu na kujikuta ikilazimika kuvunja mikataba na baadhi ya wachezaji wake katikati ya msimu huu.

Si kuvunja tu mikataba hiyo, bali pia ililazimika kusajili upya katika usajili wa dirisha dogo huku ikilazimika kubadili kocha ambaye naye amekuja na falsafa na mfumo wake ambao unamfanya kutowakubali baadhi ya wachezaji wa muda mrefu na wapya. Aidha, tunaona ni vema pia kwa klabu zilizopo katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho (FA cup), ambayo bingwa huiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa, kuwa na subra kwanza ya usajili hadi mwishoni mwa msimu.

Na kama zitasajili, basi zifanye usajili wa malengo kulingana na mashindano yaliyopo mbele yao ili zitakapobeba jukumu la kuipeperusha bendera ya nchi zisifanye tena makosa kwa kuishia hatua ya awali ya michuano hiyo.


Tunafahamu Simba inanafasi kubwa ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu kutokana na kuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti ya pointi 17 wakati huu ikiwa imebakiza michezo 10 kumaliza ligi hiyo. Na endapo ikitokea hivyo, ni dhahiri itaiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini pia kama ilivyo kwa Yanga na Azam moja kati ya timu hizo zinazopewa nafasi ya kubwa ya kutwaa Kombe la FA na kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, Simba nayo ina nafasi hiyo.

Hivyo, klabu hizi zinapaswa kutuliza akili na kufanya usajili ulioenda shule kwa kutazama wachezaji wenye viwango na uzoefu mkubwa na mashindano ya kimataifa.

Mwisho pamoja na kutazama viwango na uzoefu, lakini pia tunatarajia kuziona klabu hizo zikisajili wachezaji kulingana na mapengo yaliyopo kikosini na si kubomoa kikosi kizima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# TFF iunganishe ligi msimu huu na ujao

**KWA** sasa viongozi wa soka duniani wanakuna vichwa vyao jinsi watakavyomaliza Ligi Kuu msimu huu wa 2019/20 ambao umekumbwa na tatizo la mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

Kila nchi, viongozi wao wanakaa na kuangalia jinsi gani watamaliza mechi zilizobaki. Tayari England imeshasema kuwa ligi haitachezwa hata ikifika Aprili 30, mwaka huu kama walivyotangaza awali.

Hii inatokana na kwamba wanaona bado kutakuwa na tishio la ugonjwa huo unaoitesa dunia, wakati huu barani Ulaya kwa sasa kukionekana ndiko kumeathirika zaidi na vizuri hivyo.

Kuna wanaotaka ligi za msimu huu zifutwe na zianze upya kwa sababu huko mbele muda utakosekana wa kuchezwa mechi zilizobaki, halafu kuwe na maandalizi na msimu mpya. Wengine wanataka timu zinazoongoza ziwe mabingwa na zipewa makombe yao, huku zilizo chini zishuke daraja.

Wengine wanashauri kuwa wanaoongoza wawe mabingwa, lakini wale waliotakiwa kushuka daraja wasiteremshwe, badala yake zipandishwe timu zingine na kuwe na idadi kubwa ya timu kwa msimu ujao, lakini ligi itakapochezwa, kama huwa zinashuka tatu basi zishuke sita, na kama kuna nchi zinashuka nne, basi zishuke nane.

Hii ni mitazamo ya baadhi ya viongozi na mashabiki wengi wa soka duniani ambayo inatofautiana.

Hapa Tanzania ilitangazwa ligi kusimamishwa kwa siku 30 ili kupunguza maambukizo ya virusi vya corona kwa mashabiki ambao huwa wanajazana uwanjani, lakini pia kusitishwa hata mikusanyiko mingine mbalimbali.

Inawezekana katikati ya Aprili kama ilivyosema Bodi ya Ligi kuwa inaweza kuchezwa bila mashabiki. Hiyo inategemea na taarifa za serikali itakapokuwa imepokea mrejesho kutoka kwa madaktari na wataalam kuwa mechi zinaweza kuchezwa kukiwa na kundi dogo la watu, au watu wakusanyike sasa kwa sababu tishio halipo tena, au kuendelea kusimamishwa na siku nyingine zaidi.

Vyovyote vile itakavyokuwa, lakini hakuna uhakika wa moja kwa moja kama Ligi Kuu Tanzania Bara inaweza kuchezwa katikati ya Aprili. Kama itakuwa hivyo Mungu ashukuriwe sana.

Katika safu hii leo nataka niwape wazo Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB). Wazo langu siyo kama wale wanaotaka timu zinazoongoza zipewe ubingwa au ligi zifutwe la hasha.

Kama hadi Aprili hakutokuwa na ligi na ikaanza kuchezwa mwezi Mei kwa ajili ya kumalizia mechi zilizobaki, basi wakati inamalizia, itengeneze tu ratiba ya msimu ujao na itoe mwezi moja tu wa mapumziko kwa timu kujiandaa kabla ya msimu ujao, badala ya miwili kama ilivyo kawaida.

Huko nyuma, ligi humalizika mwishoni mwa Mei na msimu mpya huanza katikati au mwishoni mwa Agosti. Kutokana na dharura hii, mechi za msimu huu kama zitaendelea Mei, zinaweza kumalizika Juni na wachezaji wakapumzika Julai tu, kabla ya kurejea tena kwenye msimu mwingine.

Ikumbukwe kuwa tayari wachezaji wameshapumzika sasa yapata mwezi na bado wanaendelea, hii ni sawa tu na ule muda wa mapumziko ya kumalizika kwa Ligi Kuu, hivyo sidhani kama wakirejea kuna haja tena ya kuwapa mapumziko marefu tena.

Wakati ligi inafikia ukingoni tayari iwe imeshafungua dirisha la usajili kwa klabu za Tanzania ili ziweze kufanya hivyo kwa wakati unaotakiwa ili kuwezesha ligi kuanza mapema. Hii inaweza kuwa muarobaini wa kutafunwa kwa muda ambao ligi zilisimama kwa sababu ya mlipuko wa corona.

Vinginevyo tunaweza kushuhudia Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao ikianza kuchezwa mwishoni mwa Septemba au Oktoba.

Pamoja na yote hayo, tunaomba tu Watanzania waendelee kujikinga na ugonjwa huu, ili kusiwe na maambukizo mapya ambayo yanaweza kusababisha kuendelea kusimamishwa shughuli mbalimbali za kijamii na za mkusanyiko, husuan mechi za mpira wa miguu.

Kurejea mapema au kuruhusiwa kwa Ligi Kuu na Kombe la FA kutategemeana na watu wote, wakiwamo mashabiki wa soka wanavyojikinga na ugonjwa, kuzuia maambukizo mapya, ni hayo tu kwa leo.

# Turejeshe ushirika wa zamani

***Mhariri,***

*NITAJE hususan miaka ya 1970 na 1980, nikikumbuka vyema namna gani ushirika ulipamba moto nchini kote katika mustakabali wa namna mbalimbali.*

*Ninasema upana wake ulianzia katika vikundi vya wakulima na wafanyabiashara wanaoambatana nao katika namna moja au nyingine.*

*Ilipofika katika kipindi cha mageuzi katika mfumo wa ndani wa kiuchumi, kulishuhudiwa aina fulani ya mabadiliko makubwa ya huria zaidi katika mustakabali mpana wa uchumi na biashara kitaifa.*

*Ni hali iliyoendana na kususua sekta ya ushirika, ambayo baada ya juhudi za miaka mingi katika maboresho, sasa imeibuka upya. Hapo ndipo linapokuja swali au kiulizo cha kimantiki.*

*Tofauti na namna ilivyokuwa zamani, ustawi wa ushirika ukitamka sekta mtambuka kama nilivyodokeza mwanzo, hivi sasa sehemu kubwa ya ustawi wake ni katika sekta ya fedha, hapo nikimaanisha ushirika wa kuweka na kukopa, maarafu 'saccos.'*

*Ni ustawi ambao leo hii haufanani na huko ilikotokea, ikigusa kila sura za kisekta. Hivi sasa inagusa mazingira mbadala pekee ya watu kuwezeshana kukopa fedha na kunufaika nazo katika sura moja au nyingine, kwa mujibu wa malengo waliojipangia.*

*Kwa mtazamo, waratibu wote wanaosimamia ushirika kitaifa, wajaribu kuliangalia hilo na ili iwezeshwe kuinuka katika mageuzi yenye sura pana, ibebe sura ya ushirika uliokuwapo katika zama zilizopita nchini.*

***Deusdedit Nyoni,***
***Safarini Mbinga.***

# Viongozi Yanga, GSM washirikishane majukumu




**Na Adam Fungamwangu**

KUMEIBUKA sintofahamu kati ya baadhi ya viongozi wa Yanga na wadhamini wao GSM uliosababisha baadhi ya viongozi wa Kamati ya Utendaji ndani ya klabu hiyo kuenguliwa madarakani na wengine kujiuzulu.

Machi 27, mwaka huu Kamati ya Utendaji ya Yanga iliwachukulia hatua za kinidhamu Salim Rupia na Frank Kamugisha, lakini siku hiyo hiyo, wajumbe watatu ambao ni Rogers Gumbo, Shija Richard na Said Kambi walijiuzulu.

Kwa maana hiyo kwa siku moja tu tayari wajumbe watano walijiuzulu. Wimbi hili lilitokana na wanachama wengi wa Yanga kuwajia juu viongozi wao kuwa wanamzuia mdhamini wao, Kampuni ya GSM kufanya kazi yake kwa ufanisi na kuwataka wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa wote waliohusika, la sivyo viongozi wa ngazi ya juu wataubeba msalaba huo.

Wanachama na mashabiki wa Yanga walikuja juu baada ya Kampuni ya GSM kuandika barua ya kujitoa udhamini kwenye masuala yasiyo ya kimkataba ndani ya klabu hiyo.

GSM, imekuwa ikitoa mishahara kwa baadhi ya wachezaji na kusajili pia, kutoa posho na mambo mengine ambayo awali hayakuwapo ndani mkataba baina ya pande hizo mbili.

Barua hiyo baada ya kuvuja kwenye redio na mitandao ya kijamii ilizua mtafaruku kwa wanachama na wapenzi wa timu hiyo, kwani GSM baada ya kufanya mambo hayo, Yanga imeonekana kurudi kwenye heshima yake, lakini hata kiwango cha timu kimeimarika.

Wanachama na mashabiki wa Yanga, wakajua fika kuwa kama GSM wakijiweka kando kwenye masuala hayo, basi timu itarejea kule kule kwenye kusajili wachezaji wa kuungaunga, na hata mishahara ya wachezaji kuwa shida, huku yote hayo, mwisho wake hata ushindi utapatikana kwa tabu.

Inadaiwa kuwa baadhi ya wajumbe wa Yanga wamekuwa wakitilia shaka hilo la GSM kufanya kazi ambayo ipo nje ya mkataba wao kama vile kusajili wao bila kuwashirikisha viongozi, na mambo mengine ambayo yanatakiwa kufanywa na uongozi.

Kwanza kabisa mimi binafsi sijajua kama wale waliosimamishwa na waliojiuzulu wenyewe wako kundi moja au la.

Inawezekana waliosimamishwa ni wale wanaompinga GSM, lakini hawa waliojiuzulu wenyewe wamefanya hivyo kupinga wenzao kusimamishwa, au walikuwa kundi moja? Tukiondoka hapo ni kwamba kinachoonekana hapa ni mgongano wa kimadaraka na si kitu kingine chochote kile.

Ni kweli hakuna kiongozi yeyote mpenzi wa Yanga ambaye haungi mkono kinachofanywa na GSM, lakini ni kwamba ni lazima utaratibu ufuatwe.

Hata kama huna kitu nyumbani na rafiki yako anataka kukusaidia, busara itamtuma kukupa wewe pesa na kwenda kununua mahitaji ya nyumbani na si yeye kwenda kununua mahitaji na kupeleka nyumbani moja kwa moja. Hii itakuwa haileti picha nzuri kwa mke na watoto ambao wataona kuwa unasaidiwa na rafiki yako, hivyo kuanza kukudharau. GSM ilibidi watoe pesa na kuwapa viongozi ili wasajili kwa ajili ya kulinda heshima ya viongozi, vinginevyo hata wachezaji wa Yanga watakuwa wanawaheshimu GSM tu na si viongozi.

Nadhani hilo ndilo baadhi ya wajumbe walikuwa wameliona na wanalitaka lifanyike, badala ya wadhamini kufanya kazi ambayo ilitakiwa ifanywe moja kwa moja na viongozi. Tukienda kwa upande wa pili, tatizo ni kwamba viongozi wengi wa klabu za Kibongo hawaaminiki.

Nafikiri GSM inaona kama ikiwapa moja kwa moja pesa kwa ajili ya kusajili wachezaji, basi kuna baadhi ya viongozi watapiga panga kwa lugha ya kimichezo, lakini kwa ile ya kawaida ni kwamba mchezaji hazimfikii zote.

Kwenye soka kuna watu wa kati, wengi wao ni viongozi, ambao wamekuwa wakienda kwa wadhamini na wafadhili kuchukua pesa za usajili, wakisema mchezaji anahitaji Sh. milioni 50 kwa mfano, lakini mchezaji zinaweza kumfikia Sh. milioni 20 tu na 30 wanagawana wao.

Inawezekana hiki ndicho kinachomtisha GSM na kuamua yenye mwenyewe kuingia kazini, ingawa kiukweli haikutakiwa kufanya hivyo. Sasa hapa kinachotakiwa ni pande zote mbili kukaa na kuangalia ni utaratibu gani utatumika ili pande zote mbili zihusike kwa wakati mmoja kwenye masuala ya usajili na hata yale ambayo yapo nje kimkataba.

GSM na viongozi wa Yanga inabidi washirikishane kwa mambo yote ambayo yanataka kufanyika siyo mmoja wanamficha mwenzake, au kila upande unafanya mambo kivyake wakati wote lengo lao ni moja tu, kusukuma gurudumu la Yanga mbele.

Haileti picha nzuri, wote wanajenga nyumba moja, lakini wananyang'anyana fito. Kila mmoja afanye kazi yake. Viongozi wafanye kazi yao ya kuongoza klabu na GSM ifanye kazi yake iliyo ndani ya mkataba.

Na chochote kile ambacho kiko nje ya mkataba na kina manufaa kwa Yanga, ni lazima GSM iwaite viongozi wa Yanga na kuwashirikisha na kufanya maamuzi kwa pamoja, ili kila mmoja ajione ni sehemu ya mafanikio. GSM waone pesa yao imetumika kama ilivyopangwa na haijachakachuliwa, huku viongozi nao wakipewa hadhi yao ya kusajili wachezaji kama ilivyo kawaida.

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA
NA MAONI YA MSOMAJI,
UNAWEZA KUTUMA
KUPITIA KWA MHARIRI
S.L.P. 31042,
DAR ES SALAAM AU
mhariri@nipashe.co.tz

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Sumaye apewa kadi kimya kimya CCM kisa corona

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TISHIO la ugonjwa wa corona limesababisha kusitishwa kwa sherehe za kukabidhiwa kadi ya uanachama wa Chama Cha Mapinduzi(CCM), Waziri Mkuu mstaafu, Fredrick Sumaye.

Kutokana na hali hiyo, CCM imelazimika kufanya makabidhiano hayo kimya kimya bila kuwapo na shamrashamra zozote kama ilivyozoeleka.

Akizungumza jana katika hafla hiyo fupi, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alisema bila kuwapo na ugonjwa huo pangechimbika.

Alisema chama kila kinapoongeza mwanachama mpya huwa ni shughuli na sherehe kubwa na walishajipanga lakini kutokana na matatizo ya corona wameshindwa kufanya sherehe ya kumpokea Sumaye.

"Tulishajipanga, lakini kutokana na matatizo ya corona, pangechimbika hapa na tungeitangazia Dunia na hiyo sherehe hata kama ni mwaka kesho Mungu akijalia hali ya hewa ikatengemaa nakuahidi Mzee Sumaye Mungu atuweke hai sote tutafanya sherehe kubwa," alisema.

Alisisitiza sherehe hiyo haijafutwa bali imesitishwa kutii maelekezo ya serikali ili kulinda afya za wananchi wake.

Aliuagiza Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), kupitia kamati za siasa ngazi zote kuhimiza Watanzania kutii masharti ya wataalamu wa afya kuhusu kupambana na ugonjwa huo.

Hata hivyo, alisema bado kunahitaji nguvu ya elimu ya kupambana na ugonjwa huo kwenye masoko na kuwaomba Watanzania waendelee kuwa watulivu katika vita ya corona kwa kufuatilia taarifa za nchi nyingine bila kutishana.

Akizungumza kuhusu ujio wa Sumaye, alisema: "Mzee Sumaye anapata kadi na kuwa mwanachama, nakukaribisha sana Sumaye, nilikupokea Lumumba kwa niaba ya Kamati Kuu ya CCM na leo nakukabidhi kadi karibu sana nyumbani."

Alisema wastaafu bado wapo kazini na wastaafu wengi wapo CCM na Sumaye ameongeza idadi ya wastaafu ndani ya chama.

Aliongeza "Nilimuuliza Mzee Sumaye kwanini ameamua kuchagua tawi la kujiunga na CCM liwe Mji mpya jijini Dodoma, badala ya Hanang nyumbani alikozaliwa, alisema angependa kulinda historia yake kwa kuwa awali uanachama wake aliupata hapa hapa Dodoma na anatamani kuendeleza historia yake."

Akizungumza baada ya kukabidhiwa kadi hiyo, Sumaye alisema atazungumza zaidi kwenye sherehe kubwa itakayoandaliwa baada ya corona kuisha na ataomba azungumze kabla ya mgeni rasmi wa siku hiyo.

"Mmenipa heshima kubwa nashuruku tawi la Mji mpya kwa kunikubalia kuwa mwanachama bila kupewa adhabu au kukataa maana ingekuwa mwisho wa jitihada zangu za kurudi CCM, nilipohama CCM nilisema sina kinyongo wala chuki na kiongozi yeyote wa chama au mgombea nafasi ya urais.

"Nilisema naondoka CCM, lakini sina chuki na chama, Mwenyekiti wa Chama Jakaya Kikwete, wala mgombea aliyeteuliwa kugombea kiti cha urais John Magufuli, sasa wakati mwingine nitasema kwanini niliyasema haya," alisema.

Aliahidi kuwa mwanachama mwadilifu kwa kujenga chama na nchi kwa ujumla.

"Yalipotokea ya kuhama nikasema Mungu wangu vingunge hawa wametoka sasa nitafanyaje, nilisononeka, lakini ikabidi nikubali ... Lakini mimi napata furaha sana maana awali mlinipa wakati mgumu kama mdogo wenu," alisema.

## Choroko tani 52 zataifishwa

**Na Anthony Grevas,** MWANZA

SERIKALI wilayani Magu mkoani Mwanza, imekamata tani 52 za mazao ya choroko kisha kutaifishwa, zilizokuwa zikisafirishwa kwa lengo la kupelekwa jijini Dar es Salaam bila vibali vya kununulia na kusafirishia mazao hayo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Philimon Sengati, mazao hayo jamii ya mbegu na mikunde, yalikamatwa yakiwa yanasafirishwa kwenye malori matatu tofauti, likiwamo lenye tani 30, lingine tani 15 pamoja na la tani saba.

"Tulifanikiwa kuyakamata magari matatu bila kuwa na vibali vya kununulia wala kusafirishia mazao ya choroko, kinyume cha sheria, lakini tumeyataifisha kisha magari yote tumeyatoza faini ya jumla ya shilingi milioni milioni tatu...maana yake kila moja faini yake ni shilingi milioni moja," alisema.

"Baadaye tunasubiri mazao hayo kuyapeleka kwenye maghala ya vyama vya msingi vya ushirika vya mazao (Amcos) ili yakauzwe kupitia mtandao kwa njia ya mnada," akieleza na kuongeza:

"Lakini kati ya magari hayo, moja lenye tani 30 tulilikamatia mjini hapa likiwa na walanguzi waliobainika kuwa wanatoka Zanzibar."

Alisema katika Wilaya ya Magu hivi sasa biashara ya ulanguzi wa mazao kwa wakulima imekithiri, hivyo lazima watendaji wa serikali wanatakiwa kushirikiana kusimamia mazao ya wakulima ili kuwasaidia kunufaika na zao la choroko.

Mkuu huyo wa wilaya alisema biashara za ulanguzi zinaendelea kuwanyonya wakulima bei ya mazao yao, na kuwa wakinunua kilo moja kwa shilingi 600 hadi 700, badala ya wakulima kuuza kupitia vyama vya ushirika kwa njia ya mnada kupitia mtandao wanauza kwa shilingi 1,300 kwa kilo moja.

Walanguzi wamekuwa wakiisababishia halmashauri ya wilaya hiyo kupoteza mapato yake ya ndani, ukiwamo ushuru wa asilimia tatu kutokana na kuihujumu serikali kwa kukwepa kulipia ushuru wake.

Alisema kuwa wanunuzi wa mazao hayo wanatakiwa kununua kwa kufuata taratibu, sheria na miongozo ya serikali bila shuruti badala ya kuendelea kuwanyonya wakulima.



Wakazi wa Kijiji cha Kibutuka, Kata ya Kibutuka wilayani Liwale mkoani Lindi, wakitengeneza moja ya barabara za kijiji hicho juzi, ambayo imeharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Dereva bodaboda afa maji akifanya mazoezi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa mjini hapo, Salehe Azizi, anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka kati 24-25, amefariki dunia wakati akifanya mazoezi ya kuogelea kwenye ufukwe wa Bahari ya Hindi.

Mashuhuda wa tukio hilo, waliiambia Nipashe kuwa Azizi alikutwa na umauti wakati akifanya mazoezi hayo, asubuhi ya Machi 28, mwaka huu.

Baadhi ya mashuhuda hao, Issa Dadi, Rehema Ismaili, Somoe Abdallah na Daudi Hemedi, walisema siku ya tukio, Azizi akiwa na pikipiki yake alifika eneo hilo la fukwe na kuegesha pikipiki yake na kubadili nguo zake za mazoezi.

Walisema, alianza kufanya mazoezi mbalimbali ya mwili, yakiwamo ya kukimbia kando ya ufukwe huo.

"Alipofika alisimamisha pikipiki yake pale na baadaye alibadilisha nguo na kubaki na bukta na kuanza kufanya mazoezi na kukimbia," alisema mmoja wa mashuhuda hao.

Walisema baada ya kumaliza mazoezi hayo aliingia kwenye maji kwa lengo la kuondoa jasho, na ndipo umauti ulipomkuta na kufa papo hapo hadi mwili wake ulipochukuliwa na polisi na kuupeleka Hospitali ya Mkoa Sokoine kwa taratibu zingine za kitaalamu.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Sokoine, Dk. Mohamedi Muhaji, alikiri kupokea mwili huo na kuufanyia uchunguzi na kueleza kifo chake kilitokana na kubanwa na pumzi.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Foka Dinya, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho.

HABARI KITAIFA

# Mifugo inayochungiwa mjini kutaifishwa

**Na Anthony Gervas,**
MWANZA

SERIKALI wilayani Magu mkoani Mwanza imetangaza kukamata mifugo inayochungiwa mjini humo na kuitaifisha.

Aidha, itapigwa mnada ama kuipeleka machinjioni kuchinjwa ili nyama hiyo wagawiwe wanafunzi shuleni kutokana uharibifu wa mazingira.

Hatua hiyo ilitangazwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Philiomon Sengati, baada ya wafugaji kuendelea kukaidi marufuku ya mifugo hasa ya ng'ombe na mbuzi kuchungiwa katika maeneo ya mjini au kuzurura mtaani.

"Natangaza mifugo tutakayoikamata ikichungiwa mjini hapa ng'ombe na mbuzi, tutaitaifisha kisha kuiuza mnadani kama haitoshi tutaipeleka machinjioni kuchinjwa na nyama zitagawiwa shuleni wale wanafunzi kwa sababu inaharibu mazingira," alisema.

"Tumekuwa tukiikamata mifugo hiyo na kuitoza faini... mfano ng'ombe mmoja Sh.10,000, mbuzi Sh. 5,000, lakini bado wafugaji hao wanaendelea kuchunga na kukaidi agizo la serikali," alisema, Sengati. Sengati alisema kuwa kama haitoshi kuipiga mnada, serikali itaikamata na kuipeleka machinjioni kuchinjwa na nyama zake kugawiwa shuleni ili wale wanafunzi, kwa sababu bila kufanya hivyo wafugaji hawatakuwa na uchungu na kutunza mifugo yao," alisema. Hata hivyo, alisema kuwa serikali inaendelea na mkakati kabambe wa kuhakikisha wafugaji wanabadilisha maisha yao kila mmoja kwa kupatiwa ng'ombe wa kisasa zaidi pamoja na kuboreshewa majosho yao.

Aliwataka wafugaji kutii sheria bila shuruti, huku akiwataka watendaji wa serikali wakiwamo wa vijiji na kata kuhakikisha wanasimamia kikamilifu zoezi hilo hususan kuwabana wale wanaoendelea kukaidi sheria.



Mgambo wa Jiji la Dodoma wakibomoa maeneo ya miundombinu ya mifereji iliyozibwa na wafanyabiashara wa Soko la Sabasaba na kusababisha kutopitisha maji. **PICHA PETER MKWAVILA**

## Benki ya TPB yasaidia ujenzi wodi Bugando

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

BENKI ya Posta Tanzania (TPB) imetoa msaada wa tani 10 za saruji kwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando ili kuchangia ujenzi wa wodi ya wagonjwa wa saratani.

Imesema imefanya hivyo kwa kutambua ongezeko kubwa la wagonjwa wa kansa katika jamii hususani Kanda ya Ziwa.

Akizungumza wakati akikabidhi msaada huo kwa Mkurugenzi Mkuu wa hospitali hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi, alisema wanatambua hospitali hiyo inahudumia mikoa minane ya Kanda ya Ziwa na Magharibi yenye watu zaidi ya milioni 18, hivyo benki hiyo imeamua kutoa msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 3.6 utasaidia na kusogeza ukamilishaji wa ujenzi wa wodi hiyo itakayokuwa na ghorofa tatu.

Alisema ni vyema hospitali zingine kubwa zifikilie kuanzisha huduma mbalimbali kama za saratani ili kuwapunguzia wananchi adha ya kwenda jijini Dar es Salaam kwani siyo wote wana uwezo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali hiyo, Prof. Abel Makubi, alisema ongezeko kubwa la idadi ya wagonjwa wa saratani linaonyesha jinsi ugonjwa huo ulivyo changamoto katika jamii na eneo lote la Kanda ya Ziwa, kwani huduma ya saratani hospitalini hapo ilianza kutolewa mwaka 2009 ambapo jumla ya wagonjwa 320 walipatiwa huduma hadi kufikia 2019, ambapo idadi iliongezeka na kufikia wagonjwa14,000.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha miaka 10, jumla ya wagonjwa 47,000 wamepata huduma na wapo kwenye ufuatiliaji.

# Adaiwa kujifungua, kutelekeza kichanga chini ya mgomba

**Na Suleiman Rashid Omar,**
PEMBA

MKAZI wa Shehia ya Jombwe Muambe, Mkoa wa Kusini Pemba, anayekisiwa kuwa na umri wa miaka 25, amejifungua kichanga kando ya ziwa kwenye shamba la migomba kisha kukitelekeza chini ya mgomba huo.

Imeelezwa kuwa mtuhumiwa alikitelekeza kichanga hicho kuanzia saa 11 jioni hadi kesho yake saa 12 alfajiri, na kuwa kilikuwa hai.

Aidha, kilikutwa kimetandikiwa majani ya mgomba na kunyeshewa na mvua usiku kucha.

Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Zanzibar, Shadia Mohamed Suleiman, ambaye alifika kulishuhudia tukio hilo, alisema ni ajabu kumkuta mtoto huyo akiwa hai, kutokana na mazingira aliyokutwa akiwa ametelekezwa.

"Kwa kweli tumelazimika kumpa jina la Rehema kwa kuwa kupona kwake ni rehema tu kutoka kwa Mwenyezi Mungu," alisema Naibu Waziri Shadia.

Alisema kichanga hicho kilitarajiwa kusafirishwa kumpelekwa katika nyumba ya kulelea watoto iliopo Mazizini kuungana na wengine watatu, ambao nao walitelekezwa katika maeneo tafauti kisiwani Pemba, akiwamo aliyeokolewa na mbwa eneo la Pujini.

Waziri Shadia alisema kichanga hicho kilikuwa katika Hospitali ya Abdalla Mzee mkoani kikipatiwa matibabu chini ya uangalizi wa ofisa ustawi wa jamii.

Alikemea vikali tabia hio ya wanawake kujifungua watoto kisha kuwatupa.

Othuman Ame Kombo, shuhuda, alisema alikuwa kwenye eneo hilo alfajiri akitoa mitego yake ya samaki akasikia sauti ya mtoto mchanga ikilia, awali hakushtuka, lakini baadaye alishtuka ndipo alipokwenda na kukiona kichanga hicho kikihangaika.

"Baada ya kushangaa nilikwenda kuita watu, ndipo walipokuja wanawake wakakichukua na kikivika nguo na kumjulisha sheha," alisema othuman. Sheha wa Shehia ya Jombwe Muambe, alisema tukio hilo limetokea katika kijiji cha kwa Sanani Muambe ambapo mama huyo baada ya kujifungua chini ya mgomba, alimfunika mtoto jani kisha kumuacha hapo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Ahmed Khamisi Makarani, aliesema Jeshi la Polisi limeshamtambua mama wa kichanga hicho, na kwamba linamwandalia mashtaka.

Baba mzazi wa mama wa kichanga hicho, alisema hawakuwa na taarifa kama mtoto wao alikuwa mjamzito.

# AICT yatangaza utaratibu wa Pasaka

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

KANISA la Africa Inland Church Tanzania (AICT), limesema maadhimisho ya Pasaka mwaka huu yataadhimishwa katika makanisa ya mitaa ili kuepuka mikusanyiko inayoweza kusababisha maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Hayo yalibainishwa na Katibu Mkuu Kiongozi wa Afrika Inland Church Tanzania (AICT) Makao Makuu, Mchungaji Josephales Mtebe, alipokuwa akizungumza na wanahabari. Alisema katika kuunga mkono juhudi za serikali za kupambana na ugonjwa huo, kanisa hilo kupitia Baraza la Utendaji la Sinod Kuu ya AICT lilikutana Machi 18-19 mwaka huu na kukubaliana kuwa maadhimisho ya Pasaka yataadhimishwa katika makanisa ya mitaa.

Mch. Mtebe alisema hatua hiyo, itasaidia kuepukana na mikusanyiko mikubwa ambayo huko nyuma walikuwa nayo kama sehemu ya utamaduni wa kanisa hilo kwa miaka mingi pamoja na kutokuwa na safari ya kwaya na mialiko ya wahubiri kutoka kanisa moja kwenda lingine. Alisema ni muhimu kuzingatia maelekezo yote ya tahadhari yaliyotolewa na yanayoendelea kutolewa na viongozi wakati huu.

Alitoa wito kwa viongozi wa siasa nchini kutoutumia ugonjwa huo kujinufaisha kisiasa badala yake waungane katika kupambana na ugonjwa huo.

Mchungaji wa Kanisa la AICT Makongoro, Mchungaji Costantine Mkandya, alisema taifa linapaswa kumtegemea Mungu kuhusiana na ugonjwa huo.

Naye Mratibu wa Injili na Misheni wa kanisa hilo, Mwinjilisti Simbitti Nkanda, alishauri kuwekwa vitakasa mikono kwenye vyombo vya usafiri.

"Tukisema ni gharama sana hatuwezi kulinganisha na gharama ya uhai wa mwanadamu mmoja kwani huwezi kuilipa mahali popote," alisema.



Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akiwasili katika jengo la Kitega Uchumi la Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) lilipo mpakani mwa Tanzania na Uganda mkoani Kagera kwa ajili ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo hilo. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Wanaokaidi kunawa mikono sokoni kunyimwa huduma

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, amewataka wafanyabiashara wanaotoa huduma mbalimbali ikiwamo kwenye masoko ya Manispaa ya Morogoro kutowapa huduma wateja wanaokaidi kunawa kwa vitakasa mikono.

Amesema watu wa aina hiyo wanapingana na agizo la serikali katika kampeni ya nchi zima ya kuhamasisha wananchi wake wachukue tahadhari ya kujikinga na maambuziko ya virusi vya corona.

Alisema hayo kutokana na baadhi ya wenyeviti wa masoko yaliyopo Manispaa hiyo kutoa malalamiko yao kwake kuhusu baadhi ya wateja wanakataa kunawa mikono na sabuni wanapofika kununua bidhaa wakidai wamenawa nyumbani.

Mkuu wa wilaya pamoja na Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini , Mourice Masala, juzi waligawa vitiririsha ndoo na sabuni zilizotolea na Mbunge wa Jimbo hilo, Abdulaziz Abood. Vifaa hivyo vilisambazwa katika maeneo ya masoko, stendi ya mabasi Msamvu, daladala, vituo vya bajaji, vijiwe vya bodaboda na maeneo ya mamalishe katika mitaa iliyopo Manispaa ya Morogoro.

Alisema kwenye baadhi ya masoko walikopita kugawa vitiririsha ndoo, wenyeviti na makatibu wa masoko hayo walitoa malalamiko kuhusu ukaidi unaofanywa na baadhi ya wateja kukataa kunawa mikono na sabuni kabla ya kuingia ndani ya soko, hivyo kukiuka agizo la serikali.

Mkuu wa wilaya alisema ni wajibu kwa wafanyabiashara, watoa huduma na wananchi kutekeleza maagizo ya serikali ya kuchukua tahadhari ya kujikinga na virusi vya corona kwa kuweka ndoo za maji na sabuni pamoja na vitakasa mikono na wananchi kuvitumia.

"Naagiza wenyeviti wa masoko ya Manispaa ya Morogoro na wafanyabiashara kutambua kuwa suala la kunawa mikono na sabuni kabla ya kuingia sokoni ama kupata huduma dukani, kwenye magari ya abiria, bodaboda na bajaji ni amri, ambaye anagoma asipewe huduma," alisema Chonjo.

Aliwataka watoa huduma wote wa mabasi ya abiria, bajaji na bodaboda kuhakikisha abiria wananawa mikono wakati wa kupanda kituo kimoja na pale anaposhukia ikiwa na kutojaza abiria ndani ya magari yao. "Yapo maeneo mbalimbali ndani ya Manispaa na kutoa elimu na matumizi ya vitakasa mikono pamoja na mwitikio uliopo bado vitiririsha ndoo ni vichache, hivyo mheshimiwa Mbunge Abood ameamua kusaidia kutoka vya kutosha na tumevigawa maeneo yenye mkusanyiko wa watu kama stendi na masokoni," alisema Chonjo.

Naye Mwenyekiti wa Soko la Kihonda Maghorofani, Rajabu Kilongola pamoja na Katibu wa Soko la Mazimbu, Mussa Mohamed, kwa nyakati tofauti walisema kuwa wateja wengi wamekuwa hawataki kunawa mikono kwa maji na sabuni, hivyo wanashindwa kutekeleza agizo la serikali ya udhibiti wa maambukizo ya corona.

# Red Cross yapewa tano elimu corona

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Halmashauri za Msalala, Ushetu na Kahama Mjini mkoani Shinyanga, wamekipongeza Chama cha Msalaba Mwekundu (Red Cross) Tanzania kwa kuwapatia elimu ya namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Walisema kuwa licha ya kuwa na maofisa afya kila kata, lakini wananchi wa vijijini wengi hawajafikiwa na kupatiwa elimu ya namna ya kujikinga badala yake wamekuwa wakijifunza kupitia mitandao ya kijamii.

Retisia John, mkazi wa Halmashauri ya Ushetu alitoa pongezi hizo jana walipotembelewa na maofisa wa Red Cross na kuwagawia mabango na vipeperushi vyenye ujumbe wa namna ya kujikinga na ugonjwa wa virusi corona.

"Mbali na kuwa na ndoo zenye majisafi na salama na sabuni, lakini hatujapatiwa elimu na dalili za ugonjwa wa corona...kwa vipeperushi hivi tulivyovipata hii leo vitatusaidia kuzitambua dalili na kuwa mabalozi wazuri kwa wenzetu," alisema John.

Mayunga Mashaka, kutoka Halmashauri ya Msalala, alisema mitandao ya kijamii imekuwa ikiwapotosha kwa taarifa juu ya ugonjwa huo, na kuingiwa na hofu na kushindwa kujiamini hasa katika shughuli za uzalishaji mali kwa kuhofia kuugua ugonjwa huo.

Aliiomba serikali kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali kuangalia namna ya kuwadhibiti watu wanaorusha taarifa za ugonjwa huo, ambazo sio za ukweli ili kuwaondolea hofu wananchi hasa wale wanaoishi pembezoni mwa miji ambao imekuwa vigumu wao kupata taarifa za uhakika.

Mratibu wa Red Cross mkoani Shinyanga, Samuel Katamba, alisema kuwa elimu juu ya corona kwa Mkoa wa shinyanga imetolewa kuanzia ngazi za vijiji, kata hadi wilaya.

Hata hivyo, aliwataka wananchi mkoani Shinyanga, kuendelea kuzingatia maelekezo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kuhusiana na namna ya kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema kuwa kata mbili kati ya kata 58 zilizopo wilayani Kahama, hadi kufika leo watakuwa wameshazifikia kwa kutoa elimu ya kuchukua tahadhari ya kujikinga na corona na kuwapatia vipeperushi, ambavyo vinaonyesha dalili za ugonjwa huo.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu, Dk. Nicodemus Senguo, aliwataka wananchi kunawa mikono kwa kutumia majisafi na salama na sabuni, lakini wenye uwezo wanaweza kununua vitakasa mikono vinavyozuia bakteria.

# ILO yasitisha ajira kwa watoto milioni 152

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHIRIKA la Kazi Duniani (ILO), kwa kipindi cha miaka 16 kuanzia 2000 hadi 2016 wamefanikiwa kutokomeza ajira za watoto milioni 152 duniani.

Akizungumza jijini Arusha, wakati wa mafunzo ya mpango wa miaka mitatu wa kupambana na utumikishwaji wa watoto, Mratibu wa kitaifa wa ILO, Gerson Nyadzi, alisema idadi ya ajira kwa watoto ni kwa mujibu wa takwimu za ILO kwa dunia nzima.

Kati ya watoto waliokuwa kwenye ajira hizo, milioni 64 ni wasichana na wavulana ni milioni 88.

Alisema watoto milioni 73, walikuwa wakifanya kazi katika mzingira magumu, hatarishi na yasiyokuwa salama ukilinganisha na umri pamoja na afya zao.

Alisema bara la Afrika linaongoza kwa ajira za watoto na tathmini iliyofanyika imeonyesha kuwa kati ya mtoto mmoja mpaka watoto watano wote kwa pamoja wanatumikishwa katika ajiraB wakiwa na umri mdogo. Alisema watoto wengi wameajiriwa katika sekta ya kilimo, hususani kwenye mashamba ya zao la tumbaku.

Aidha, alisema shirika hilo kwa kushirikiana na serikali na wadau wameandaa programu ya kupambana na ajira kwa watoto pamoja na unyanyasaji wa wanawake.

"Hadi sasa idadi kubwa ya watoto wametolewa katika ajira wakiwa na umri mdogo, tumefanikiwa kutokana na hatua ya utoaji wa elimu katika jamii kuhusu madhara ya ajira kwa watoto," alisema.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2014, kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu, kwa kushirikiana na (ILO) kwenye utafiti waliofanya waligundua zaidi ya watoto milioni nne wanatumikishwa katika ajira za utotoni.

Pia alisema kwa Tanzania asilimia 29 ya watoto wenye umri kati ya miaka mitano hadi 17, wanafanya kazi katika shughuli za kiuchumi, ikiwamo kilimo, kazi za nyumbani, uvuvi na migodini.

"Tangu mwaka 2001, serikali ya Tanzania imeridhia makubaliano ya kupambana na ajira za watoto kwa mujibu wa azimio la Shirika la Kazi Duniani ya haki za watoto namba 138 ya mwaka 1973.

Mwakilishi kutoka Chama cha Waajiri nchini (ATE), Vitus Lugakingira, alisema chama hicho, kimekuwa kikishirikiana na serikali kupiga vita ajira kwa watoto.

"Tutahakikisha tunashirikiana na serikali na wadau mbalimbali kupambana na ajira kwa watoto," alisema Lugakingira.



Maofisa Ustawi na Maendeleo ya Jamii wa Mkoa wa Arusha wakifuatilia mada zilizokuwa zikitolewa wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa wa corona jijini Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: RAYMOND ISHENGOMA**

# Watumishi afya wanolewa corona

**Na Allan Isack,** BABATI

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa nchini, (TALGWU), kimetoa mafunzo kwa watumishi wa kada ya afya, katika Hospitali ya Dareda iliyopo Wilaya ya Babati mkoani Manyara.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha matumishi hao kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa.

Katibu wa TALGWU Mkoa wa Manyara, Ndulilah Pandauyaga, alisema chama hicho kimetoa mafunzo hayo, kwa ajili ya kuwaelimisha watumishi kitengo cha afya.

Alisema chama hicho kina wa wanachama wengi, hivyo wametoa mafunzo hayo endapo mlipuko wa ugonjwa wa corona utatokea wasiwapoteze wataalamu hao.

Alisema wauguzi wakijilinda na wasipopata maambukizi ya ugonjwa huo, ni jambo jema kwa afya zao, na kwamba pia wananchi watakuwa na matumaini makubwa wakati wakipatiwa matibabu kwa kuwa watakuwa na uhakika wa kupona.

Naye Katibu wa Afya Wilaya ya Babati, Suten Mwambulambo, alisema ni vyema wataalamu wa afya kujikinga kwanza wao na familia zao.

Joseph Lorri, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Dareda, alisema mafunzo hayo yamewafundisha kuwa makini wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa ili wasipate maambukizi ya ugonjwa huo. Mafunzo hayo, yalijumuisha watumishi wote wa hospitali ya Dareda, wauguzi, madaktari, walinzi, mafundi pamoja na wafanya usafi katika hospitali hiyo.

Aidha, alisema barakoa na vitakasa mikono vimekuwa ni adimu kupatikana kwa sasa, lakini awali kabla ya kutokea kwa ugonjwa huo walikuwa na vitu hivyo, na vilikuwa vikitumiwa na wafanya usafi hospitalini hapo pamoja na madaktari wakati wakufanya upasuaji wa wagonjwa.

"Tumejaribu kutafuta vitakasa mikono na barakoa kwa wafanyabiashara wanaosambazaga mitaani, wanasema kwa sasa vifaa hivi havipatikani, na sisi hatufahamu tutakwenda kuvipata wapi, na wakati mwingine ukipata bei inakuwa kubwa," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Wilaya hiyo, Dk. Madama Hosea, alikiri kuwa kuna upungufu wa dawa pamoja na vitakasa mikono, hivyo alisema wamewasiliana na Bohari Kuu ya Dawa ili kupatiwa dawa na vifaa.

Alisema wanatarajia baada ya muda mfupi dawa na vifaa hivyo, vitaletwa kwa kuwa tayari wameshaomba.

# CCM yaagiza kijiji kujenga ofisi ya walimu

**Na Allan Isack,** BABATI

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi(CCM) Wilaya ya Babati mkoani Manyara, imeiagiza serikali ya Kijiji cha Minjingu kujenga ofisi ya walimu katika Shule ya Msingi Minjingu.

Lengo la agizo hilo ni kuzuia walimu wasitumie darasa kama ofisi yao.

Ujenzi huo pia utasaidia walimu wa shule hiyo kutokufanyia shughuli zao chini ya miti.

Agizo hilo, lilitolewa na kamati hiyo wakati wa ziara yao ya kikazi kukagua miradi ya maendeleo wilayani humo.

Katibu wa CCM Wilaya ya Babati, Filbert Mapwepwe, amemtaka mwenyekiti wa kijiji hicho kukaa na serikali ya kijiji kuangalia namna ya kuwajengea walimu ofisi ili wasitumie darasa kama ofisi ya kufanyia kazi.

"Nitakuja hapa tena Aprili kuangali kama mmeshaanza ujenzi wa ofisi hiyo, maana wanafunzi hawawezi kuteseka kwa kukaa chini kutokana na walimu kutumia darasa lao kama ofisi," alisema Mapwepwe.

Baada ya kutoa maagizo hayo, walikagua madarasa matatu na matundu 24 ya vyoo vya shule hiyo, ambayo wamejengewa na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (JUHIBU).

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Babati, Nicodemus Tarimo, alishangazwa na walimu kuligeuza darasa kuwa ofisi yao.

Tarimo alisema kilichokwamisha ujenzi ni wananchi kuwa wagumu wa kuchangia ujenzi.

Alisema tangu JUHIBU watoe fedha za ujenzi wananchi wa Minjingu, hawakuridhika na walikataa kutoa fedha za ujenzi bila ya kuwa na sababu maalumu.

Mjumbe mwingine wa kamati hiyo, Michael Tsaxara, alisema walimu kutumia darasa kama ofisi hawatendei haki kwa wanafunzi.

Akisoma taarifa ya ujenzi huo uliofadhiliwa na Juhibu, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Minjingu, Veronica Kweka, alisema mradi huo unathamani ya Sh. milioni 249.6 na fedha zilizotumika hadi sasa ni Sh. milioni. 234.

Kweka alisema shule hiyo, ina walimu 17 na wanafunzi 1,000 kuanzia darasa la awali mpaka darasa la saba.

Mwalimu Idrisa Msemo alisema shule hiyo, inaupungufu wa majengo ya utawala ndio sababu wametumia darasa kama ofisi ya kufanyia shughuli zao. Naye Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Samuel Melam, alikiri walifanya makosa kwa kutumia darasa kama ofisi ya walimu wakati wanafunzi wana uhaba wa vyumba vya madarasa.





# Waipigia chapuo sekta ya kilimo bajeti 2020/21

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WADAU wa kilimo mkoani Kilimanjaro, wameishauri serikali, Bunge la Bajeti litakapoanza rasmi Machi 31, mwaka huu, lije na vipaumbele sekta ya kilimo vitakavyofanya ifanikiwe na kuleta matokeo chanya.

Wameitaka wizara yenye dhamana kuchukua hatua ya kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili wakulima hasa wa mboga na matunda kukosa soko la uhakika nchini la kuuza mazao yao.

Akizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kuhusiana na kilio cha wakulima wa mazao ya mboga na matunda kukosa masoko, Flora Laayuni, kutoka Shirika la Kilimo la Mkulima Mbunifu, alisema bila vipaumbele na bajeti ya uhakika, kilimo kitaendelea kuwa na malalamiko.

"Tunadhani njia bora ya kumaliza au kupunguza malalamiko ya wakulima ni kushughulikia masuala kama upatikanaji mitaji, masoko, mabadiliko ya sera yasiyotabirika, miundombinu pamoja na kutokuwapo kwa mazingira rafiki yanayovutia uwekezaji," alisema Laayuni.

Kwa upande wake, Salvatory Mbuya, alisema miongoni mwa vitu vinavyotakiwa kufanyiwa kazi ili kuimarisha sekta ya kilimo ni pamoja na kuwa na mazingira rafiki ya kisera, kodi na taasisi zinazosimamia sekta hiyo.

Kwa mujibu wa Mbuya, kwa sasa kuna utitiri wa taasisi za kusimamia sekta ya kilimo jambo linalowakatisha tamaa wakulima na wawekezaji.

Jambo lingine lililozungumziwa ni kukosekana miundombinu ya uhifadhi mazao yanayozalishwa, hali inayosababisha kuharibika.

Amesema kuwa kati ya asilimia 35-40 ya mazao ya nafaka hupotea baada ya kuvunwa, huku asilimia 60 ya matunda na mboga yanaharibika na kushauri kuimarishwa teknolojia ili kuepusha hasara.

Kutokana na malalamiko ya wakulima wa mikoa ya Kilimanjaro na Manyara kukosa masoko, tayari kampuni mbili za kimataifa kutoka nchi jirani ya Kenya, zimetangaza kuingia makubaliano na wakulima wa mboga, matunda na nafaka wa vijiji vya pembezoni kati ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro na Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara.

Meneja Miradi wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Rikolto inayowasaidia wakulima nchini Tanzania kupata masoko ya uhakika, Kain Mvanda alisema kampuni hizo zipo tayari kununua tani 180 kwa mwezi.

Kampuni hizo ni Fresh Mart na Molly Flowers ya Kenya.



Mabaki ya vibanda vilivyoungua kwa moto soko la Samunge Arusha Mjini usiku wa kuamkia jana na kuacha simanzi kwa wafanyabiashara wa soko hilo. **PICHA: CYTHIA MWILOLEZI**

# Walalamika miundombinu mibovu stendi Bomang'ombe

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MADEREVA wa mabasi ya abiria katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, wameilalamikia serikali kwa kushindwa kukarabati miundombinu ya stendi ya mabasi ya Bomang'ombe.

Kituo hicho kinatumika kupakia na kushusha abiria kwa mabasi yaendayo mikoani na ndani ya wilaya hiyo.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya madereva walisema eneo hilo limesahaulika kwa muda mrefu bila kukarabatiwa.

Hassan Mbaga, ni dereva wa basi dogo linalofanya safari zake kati ya Moshi na Arusha, alisema hali hiyo imesababisha kuwapo na mashimo yanayosababisha mabasi yao kuharibika licha ya kuwa wanalipa ushuru.

Naye, Frederick Tesha alisema barabara ya kutoka na kuingia imejaa mashimo makubwa na inapitika kwa shida.

Alipotafutwa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai, Noel Nnko kuzungumzia suala hilo, alisema serikali inafanyia kazi malalamiko hayo na kuahidi kulifikisha katika mamlaka husika. Alisema kwa sasa serikali iko katika maandalizi ya ukarabati.

Kituo hicho kwa muda mrefu kimesahaulika kufanyiwa ukarabati, hali inayosababisha kuwapo kwa usumbufu wa watumiaji wa eneo hilo.

## Wakili asikitishwa wenye ulemavu kutochangamkia fursa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKILI mkongwe katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Elizabeth Minde, ameeleza kusikitishwa na idadi ndogo ya watu wenye ulemavu kuchangamkia fursa za kiuchumi katika mkoa wa Kilimanjaro.

Akizungumzia kikwazo hicho kwa wenye ulemavu, wakili huyo na mwanaharakati wa haki za binadamu, alisema kuna haja ya kutolewa elimu ya kutosha kuhusu ushiriki wao katika fursa za kiuchumi.

"Kuna shida katika kundi hili na nadhani kuna haja kwa mamlaka zinazohusika na jambo hilo kulitazama upya. Idadi ndogo ya kundi hili kujitokeza hata kuchukua mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri za wilaya ni tatizo ambalo halijaonekana," alisema Minde.

Siku chache zilizopita Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, alisema serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu Sheria Namba 9 ya Mwaka 2010 inayohusu haki na ulinzi kwa watu wenye ulemavu.

Kwa mujibu wa Warioba, serikali itaangalia namna inavyotekelezwa na hasa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa makundi maalumu.

Alisema sheria hiyo pamoja na mambo mengine inataka kuhakikisha wenye ulemavu wanapatiwa haki hiyo ikiwamo pia masuala ya ajira, elimu, afya na utengamao wa maisha yao ili kuondokana na dhana potofu ya utegemezi kwa kundi hilo.

Alisema serikali inaendelea na jitihada zake za kuwawezesha watu wenye ulemavu kwa kuwatengea asilimia mbili katika kila halmashauri, mikopo ambayo haina riba na inayolenga kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

"Ipo haja ya kila mwenye ulemavu kujitahidi kujishughulisha na shughuli ya kumwongezea kipato kwa kuzingatia uwezo aina ya ulemavu wake, kwa kuwa serikali inaendelea kuweka mkazo kuliangalia kundi hili."

"Huu ni wakati sahihi wa kundi hili kuangaliwa na kupatiwa elimu ya ujasiriamali ili waweze kujikimu katika mahitaji yao na familia zao kwa ujumla."

Nipashe
# Spotika



KLABU 10 ZENYE VIKOSI VYA THAMANI KUBWA DUNIANI UK. 16 & 17




## ISIKUPITE

JANGA la corona (COVID-19), limemchelewesha mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo kufikisha mabao 100 kwenye timu ya taifa, wakati huu akiwa na mabao 99, alitarajia kufikia idadi hiyo Ijumaa iliyopita kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Ubelgiji ama baadaye dhidi ya Croatia kabla ya mechi hizo kuahirishwa. Hadi sasa rekodi ya mabao mengi timu ya taifa inashikiliwa na Ali Daei wa Iran mwenye mabao 109.

# CORONA KUWABEBA?

Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania na klabu ya Aston Villa, Mbwana Samatta akijaribu kuchomeka kichwa dhidi ya beki wa kulia wa Bournemouth, Adam Smith katika mechi yake ya kwanza Ligi Kuu England akitokea KRC Genk ya Ubelgiji. Aston Villa iliyopo nafasi ya 19 katika msimamo wa Ligi Kuu ni moja kati ya klabu zinazoelezwa zinaweza kunufaika na kusimama kwa ligi hiyo kutokana na kasi ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19). **HABARI UK. 19**

## SOKA



# NYOTA WA3 WANAOWEZA KUMRITHI OZIL ARSENAL

**LONDON,** England

MSIMU wa kwanza wa Mikel Arteta kama kocha wa Arsenal umeingia kwenye wakati mgumu baada ya kusimamishwa kwa Ligi Kuu ya England kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

**Licha ya kutupwa nje kwenye Ligi ya Europa, 'Washikabunduki' hao wamekuwa na wakati mzuri chini ya kocha huyo msaidizi wa zamani wa Manchester City. Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 37, anajua kwamba bado ana kazi kubwa ya kufanya kuiweka klabu hiyo kwenye nafasi ya ushindani, na moja ya kazi yake kubwa ni kutafuta mrithi wa Mesut Ozil.**

Mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid alikuwa na wakati mgumu pale Arsenal baada ya ujio wa Unai Emery. Kiungo huyo aliminywa na kocha huyo wa zamani wa Sevilla na PSG, na mara zote alikuwa akichezeshwa katika nafasi ambayo si yake.

Hata hivyo, tangu kuwasili kwa Arteta hapo kwenye dimba la Emirates, Ozil amekuwa akipata nafasi ya kucheza mara kwa mara kwa miamba hao wa London Kaskazini na kiwango chake kinaonekana kuimarika.

Raia huyo wa Ujerumani ni mmoja wa wachezaji wenye vipaji vya ukweli barani Ulaya ambaye wakati akitua pale Arsenal alikuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho.

Lakini sasa ni wazi kwamba Arsenal inaonekana haipo tayari kumwongezea mkataba kutokana na mshahara wake kuwa mkubwa zaidi na ambao klabu hiyo haitaweza kuumudu.

Makala haya yanaawaangalia wachezaji watatu ambao wanaweza kuwa warithi wa Ozil pale Arsenal, watambue sasa...

**#1. ORKUN KOKCU (FEYENOORD)**

Orkun Kokcu ni zao la akademi ya Groningen na akahamia kule Feyenoord mwaka 2014 kwa ajili ya kujiimarisha zaidi. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, aliingia kwenye kikosi cha kwanza cha Feyenoord msimu wa 2018-19 na ingawa hakuwa akicheza mara kwa mara, lakini alitumia vizuri kila nafasi aliyopata.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Uturuki amekuwa nguzo muhimu kwenye safu ya kiungo ya Feyenoord akichangia jumla ya mabao matatu na kutoa pasi za mwisho ('asists') sita katika mashindano yote msimu huu.

Kokcu ni kiungo mbunifu na mzuri wa chenga ambaye anaweza kuipita safu yoyote ya ulinzi na mgawaji mzuri wa pasi. Anafiti zaidi kwenye namba 10 na kama Washikabunduki hao wataweza kumsajili kipindi cha majira ya joto, atakuwa msaada mkubwa kwao. Kutokana na umri wake wa miaka 19, atakuwa na nafasi nzuri ya kujifunza zaidi chini ya Arteta.

Licha ya kuwa na miaka miwili zaidi katika mkataba wake wa sasa, Arsenal wana nafasi ya kumsajili Kokcu kwa sababu tayari wamefunguliwa milango ya mazungumzo.

**#2. JACK GREALISH (ASTON VILLA)**

Jack Grealish, ambaye amekuwa kwenye kiwango bora zaidi pale Aston Villa ni mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu na nafasi nzuri ya kuwa mrithi wa Ozil pale Arsenal.

Muingereza huyu ana stamina ya hali ya juu na ubora wa kiwango cha juu ambacho kinaweza kubeba vizuri zaidi mikoba ya Ozil.

Hata hivyo, kwa vyovyote vile Aston Villa watahitaji kiwango kikubwa zaidi cha fedha ili kumwachia Grealish mwenye umri wa miaka 24, ambaye ndiye kipenzi cha mashabiki wa klabu hiyo.

**#3. EMILE SMITH ROWE (ARSENAL)**

Emile Smith Rowe, ambaye anatajwa kama mmoja wa wachezaji vijana anayechomoza kwa kasi pale kwenye dimba la Emirates, ambaye anaweza kuvaa vizuri na kwa muda mrefu viatu vya Ozil. 'Dogo' huyo mwenye umri wa miaka 19, amefunga mabao sita akiwa na jezi ya Arsenal na amekuwa na kiwango cha kuvutia kwa sasa akicheza pale Huddersfield Town kwa mkopo.

Kinda huyo amefunga bao moja na kutoa pasi za mwisho tatu katika mechi 10 alizoichezea klabu hiyo inayonolewa na kocha, Danny Cowley ambaye amekunukuliwa akimsifia kwa kusema: "Emile Smith Rowe kwa hakika ni mchezaji ninayempenda, ana uwezo, kasi na kiwango cha kuvutia zaidi na akiwa kwenye goli ana uwezo mkubwa wa kufunga."

Huku Arteta akiwa na mipango ya kuijenga upya Arsenal, Rowe ana nafasi nzuri zaidi ya kuwa msaada kwake na kumrithi vizuri Ozil.

**JE, WAJUA?**



MANCHESTER City ndicho kikosi chenye thamani kubwa zaidi duniani kwa sasa kikiwa na thamani ya euro bilioni 1.29, huku kikifuatiwa kwa karibu na Liverpool (euro bilioni 1.19) pamoja na Real Madrid (euro bilioni 1.08)

# MICHEZO




Mchezaji wa Simba, Miraji Athumani.. **PICHA: MAKTABA**

# CORONA ITAKAVYOWABEBA MAJERUHI HAWA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ulimwengu wa michezo ukiwa kimya kutokana na kasi ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), vilivyosababisha Ligi Kuu mbalimbali za mpira wa miguu duniani kusimamishwa, kuna ahueni imepatikana kwa baadhi ya klabu na wachezaji ambao walikuwa majeruhi.

**Kama kusingekuwapo na kasi ya maambukizi ya virusi vya corona, inawezekana baadhi wasingecheza tena msimu huu hadi ligi zinaisha na wengine wangecheza mechi chache sana, kabla ya Ligi Kuu msimu huu kumalizika.**

Kusimama kwa ligi kumewapa nao nafasi ya kupona na kuanza mazoezi huku kukiwa hakuna ligi yoyote inayoendelea na itakapoanza nao wanaonekana watakuwa fiti tayari kurejea dimbani.

Hawa ni baadhi ya majeruhi ambao huenda wasingecheza tena ligi, au kucheza mechi chache kama ligi isingesimama kutokana na corona.

**1. MIRAJI ATHUMANI- SIMBA**

Huyu ni majeruhi wa muda mrefu sasa kwenye kikosi cha Simba, hadi ameanza kusahaulika kwa wanachama na mashabiki wa klabu hiyo. Alianza kwa moto mkubwa, akipachika mabao sita kwenye mechi chache tu alizoichezea timu yake, kabla ya kuwa majeruhi.

Baadaye alipona, lakini aliumia tena kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar dhidi ya Mtibwa Sugar.

Mpaka katikati ya ligi Miraji Athumani anayecheza nafasi ya winga wa kulia au kushoto, alikuwa majeruhi na hata timu yake ikiwa imebakisha mechi 10 tu kabla ligi haijamalizika, bado hakutegemewa kama angekuwa fiti.

Katikati ya mwezi uliopita alianza mazoezi ya mepesi na kutokana na ligi kusimamishwa anaweza kuwa fiti na kuiwahi Ligi Kuu kwenye mechi zilizobaki. "Nina imani muda si mrefu nitarejea uwanjani na kuendelea kupambania timu yangu na kufanya majukumu ya kila siku," alisema.

**2. RELIANTS LUSAJO- NAMUNGO**

Hakuwapo kwenye mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Yanga, Machi 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Majaliwa Ruangwa mjini Lindi. Kwenye mechi hiyo ambayo timu ilitoka sare ya bao 1-1, Reliants Lusajo anayekamata nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji Ligi Kuu, akiwa na mabao 11 nyuma ya Meddie Kagere wa Simba, hakucheza kwa sababu alikuwa majeruhi.

"Kwa sasa bado nimepumzika, nina mpango wa kuanza mazoezi baada ya wiki moja," alisema Lusajo siku chache baada ya kupata nafuu, ikiwa ni siku chache kabla ya Ligi Kuu kusimamishwa kutokana na kuepuka maambukizi ya COVID-19.

**3. MZAMIRU YASSIN- SIMBA**

Aliumia kwenye mechi ya kwanza kati ya watani wa jadi, Simba na Yanga, Januari 4, mwaka huu miamba hiyo ikitoka sare ya mabao 2-2.Tangu hapo hadi leo hii, hajaonekana tena dimbani, lakini duru za soka zikisema kuwa kwa siku za karibuni alikuwa ameanza mazoezi mapesi na timu yake. Huenda isingekuwa rahisi sana kucheza mechi nyingi kama ligi ingekuwa inaendelea, lakini hadi itakaporuhusiwa atakuwa amepona kabisa na kuwa na uwezekano wa kucheza mechi zilizobaki.

**4. MBARAKA YUSUPH- AZAM FC**

Mbaraka Yusuph ni majeruhi wa muda mrefu zaidi. Alifanyiwa upasuaji Aprili mwaka jana nchini Afrika Kusini. Wakati huo alikuwa akiichezea Namungo FC kwa mkopo akitokea Azam FC. Habari njema ni kwamba mwezi uliopita ameanza mazoezi na timu ya Azam FC, hadi ligi itakaporejea tena, straika huyo atakuwa fiti tayari kwa kurejea tena uwanjani.

Straika huyo alikuwa anasumbuliwa na majeraha ya goti aliyoyapata akiitumikia timu ya Namungo katika harakati za kuipandisha Ligi Kuu.

**5. ERASTO NYONI- SIMBA**

Beki wa kati wa Simba na Taifa Stars ambaye aliumia wakati akiichezea timu yake dhidi ya Yanga, Machi 8, mwaka huu, wakichapwa bao 1-0.

Huenda angecheza mechi chache sana kama ligi ingeendelea, lakini kwa sababu ni tegemeo, wakati ligi inaanza itamkuta tayari amepona na kucheza mechi zilizobaki kama kawaida.

**NJE YA UWANJA**

MASTAA wa Ligi Kuu England akiwamo Raheem Sterling wameanzisha kampeni ya "Kaa Nyumbani, Kuokoa Maisha" kupitia mitandao yao ya kijamii ikiwalenga mashabiki wa soka kujikinga na kasi ya maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19).



Extra Time



# KLABU 10 ZENYE VIKOSI VYA THAMANI KUBWA DUNIANI

**LONDON,** England

KLABU za Ligi Kuu ya soka England na ile ya Hispania, La Liga, hazijawahi kusita kwenye matumizi ya fedha nyingi katika usajili. Klabu hizo zimekuwa zikitumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyake.

**Na hili limefanya ligi za nchini hiyo kuwa na ushindani mkubwa katika kuwania mataji. Hapa tunaziangalia klabu kubwa 10 zenye vikosi vya thamani zaidi sokoni kwa sasa, twende pamoja...**

**#10. MANCHESTER UNITED: EURO MILIONI 800.75**

Manchester United ni moja ya klabu maarufu zaidi duniani. Licha ya kuwa kwenye wakati mgumu kwa siku za hivi karibuni chini ya Ole Gunnar Solskjær, bado inasimama kama klabu yenye wachezaji bora duniani.

'Mashetani Wekundu' hao kikosi chao kina thamani ya euro milioni 800.75 na mchezaji wao mwenye thamani kubwa zaidi ni Paul Pogba ambaye thamani yake ni euro milioni 100. Wanaofuata baada ya Mfaransa huyo ni Marcus Rashford mwenye thamani ya euro milioni 80, Harry Maguire euro milioni 70. Na mchezaji wao mpya waliomsajili hivi karibuni, Bruno Fernandes thamani yake ni euro milioni 60.

**#9. CHELSEA: EURO MILIONI 848.05**

Chelsea imemshangaza kila mmoja kwa kiwango chake msimu huu. Licha ya kubadilishwa kwa kocha na kufungiwa kufanya usajili, Blues hao wameweza kupambana vizuri na kuendelea kupigania kwenye nne bora katika Ligi Kuu ya England.

Klabu hiyo kutoka London Magharibi kikosi chake kina thamani ya euro milioni 848.05 na N'Golo Kante ndiye mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi katika kikosi hicho, ambapo thamani yake inatajwa kuwa ni euro milioni 100. Anayefuata ni Jorginho mwenye thamani ya euro milioni 65.

**#8. ATLETICO MADRID: EURO MILIONI 863.50**

Atletico Madrid imechomoza katikati ya Real Madrid na Barcelona kwenye soka la Hispania. Kocha Diego Simeone amejenga kikosi imara na chenye ushindani mkubwa dimbani.

'Rojiblancos' hao kikosi chao kina thamani ya euro milioni 863.50 na mchezaji mwenye thamani kubwa ni Jan Oblak na Joao Felix ambapo wote kila mmoja thamani yake ni euro milioni 100. Anayefuata ni Saul Niguez mwenye thamani ya euro milioni 90 na Jose Giminez mwenye thamani ya euro milioni 70.

**#7. TOTTENHAM HOTSPUR: EURO MILIONI 897.50**

Tottenham Hotspur thamani ya kikosi chake inatajwa kuwa ni euro milioni 897.50, huku ikiwa na mjumuiko wa wachezaji wakubwa na wadogo. Uhamisho wa Christian Eriksen kwenda Inter Milan ukaifanya Spurs itie mfukoni kiasi cha euro milioni 85, lakini usajili wao mpya wa Gedson Fernandes na Steven Bergwijn wamepunguza pengo hilo.

Mchezaji anayeongoza kwa thamani kubwa pale Spurs ni Harry Kane ambaye thamani yake inatajwa kuwa euro milioni 150. Wanaofuata ni Dele Alli mwenye thamani ya euro milioni 90, Heung-min Son euro milioni 80 na Tanguy Ndombele euro milioni 65.

**#6. BAYERN MUNICH: EURO MILIONI 934.15**

Bayern Munich ndio klabu pekee kutoka nchini Ujerumani ambayo ipo kwenye orodha hii, ambapo thamani yake ni euro milioni 934.15. Serge Gnabry na Joshua Kimmich ndio wachezaji wenye thamani kubwa kwa euro milioni 80 kila mmoja. Anayefuata ni Philippe Coutinho, Robert Lewandowski na Lucas Hernandez ambapo kila moja thamani yake ni euro milioni 70.

**#5. PARIS SAINT-GERMAIN: EURO BILIONI 1.02**

Paris Saint-Germain moja ya timu imara zaidi kwenye makaratasi. Huku safu yao ya ushambuliaji ikiwajumuisha wachezaji wakali, Neymar Jr, Kylian Mbappe, Edinson Cavani, Angel di Maria na Mauro Icardi. Parisians hao ni moja kati ya timu yenye washambuliaji wakali zaidi duniani.

Miamba hao wa soka la Ufaransa kikosi chao kina thamani ya euro bilioni 1.02, huku mchezaji wake mwenye thamani kubwa zaidi akiwa ni Mbappe ambaye kwa sasa sokoni bei yake ni euro milioni 200. Anafuatiwa na Neymar mwenye thamani ya euro milioni 160, Marco Verratti na Mauro Icardi kila mmoja akiwa na thamani ya euro milioni 75.

**#4. FC BARCELONA: EURO BILIONI 1.07**

Nyumba ya FC Barcelona ina mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani kwa sasa, Lionel Messi na si jambo la kushangaza kwamba, 'Blaugrana' hao kwa sasa thamani ya kikosi chake ni euro bilioni 1.07.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, bado wanaendelea kufurahia mafanikio makubwa dimbani kwa kuwa na timu bora zaidi. Waliwasajili wachezaji wa kiwango cha juu zaidi duniani wakati wa kipindi cha majira ya joto, Antoine Griezmann na Frenkie de Jong ambao walinunuliwa kwa kitita kikubwa cha fedha.

Hakuna anayeweza kushangaa kwamba, Messi ndiye mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi kwenye kikosi hicho ambapo thamani yake ni euro milioni 140 akifuatiwa na Griezmann euro milioni 120, De Jong na Marc-Andre Ter Stegen kila mmoja ana thamani ya euro milioni 90 na Ousmane Dembele ana thamani ya euro milioni 75.

**#3. REAL MADRID- EURO BILIONI 1.08**

Real Madrid ndiyo klabu yenye mafanikio makubwa zaidi kwenye soka la Ulaya baada ya kutoka kushinda mara nne taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita. Miamba hao wa Hispania kipindi cha majira ya usajili kilichopita cha msimu wa 2018-19 ilitumia kiasi cha euro milioni 300 kuimarisha kikosi chake.

Kikosi cha Los Blancos hao kwa sasa thamani yake ni euro bilioni 1.08 na mchezaji wao mwenye thamani kubwa ni Eden Hazard ambaye thamani yake ni euro milioni 120. Anayefuata ni mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji, Raphael Varane mwenye thamani ya euro milioni 80, Casemiro euro milioni 70 na Toni Kroos euro milioni 60.

**#2. LIVERPOOL: EURO BILIONI 1.19**

Bingwa huyu mtetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya ni moja ya timu yenye kikosi cha thamani zaidi duniani ambapo ni euro bilioni 1.19.

Nyuma ya mafanikio ya Liverpool yupo kocha, Jurgen Klopp raia wa Ujerumani ambaye amekuwa na mafanikio makubwa zaidi tangu achukue mikoba ya kukinoa kikosi hicho. Wachezaji wenye thamani kubwa zaidi kwenye kikosi hicho ni Mohamed Salah, Sadio Mane na Roberto Firmino, ambapo wawili hao kila moja thamani yake ni euro milioni 150 na anayewafuatia ni euro milioni 90.

'Wekundu' hao wa Anfield pia wana safu bora zaidi ya ulinzi Ulaya ambapo inawajumuisha golikipa Alisson Beckerna mabeki Virgil van Dijk, Andrew Robertson na Trent Alexander-Arnold ambao thamani yao kila mmoja ni euro milioni 90, euro milioni 100, euro milioni 80 na euro milioni 110.

**#1. MANCHESTER CITY: EURO BILIONI 1.29**

Manchester City ina kikosi chenye thamani kubwa zaidi duniani kwa sasa. Si tu kwamba wana kundi la wachezaji bora, lakini wanapewa nguvu kubwa na kocha wao, Pep Guardiola. Tangu mkali huyo kutoka kule Catalunya achukue mikoba ya kuinoa timu hiyo pale Etihad, imetawala soka la Uingereza na msimu uliopita ilitwaa mataji matatu.

Kikosi cha Manchester City thamani yake ni euro bilioni 1.29 na mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi kikosini hapo ni Raheem Sterling mwenye thamani ya euro milioni 160 akifuatiwa na Kevin de Bruyne euro milioni 150 na Leroy Sane na Bernardo Silva wote kila moja akiwa na thamani ya euro milioni 100.

## Nukuu

"Ninamwona Mane akiwa Real Madrid [kuliko Mohamed Salah]. Yeye [Mane] ana tabia ambazo Zinedine Zidane anazitaka... Nadhani Mane atakwenda Real Madrid, sijui kama Salah ataendelea kuwapo Liverpool. Lakini kama Salah ataondoka, kuondoka kwake itakuwa vizuri kwa timu, Liverpool ni wazuri sana na watajua namna ya kuziba nafasi yake," **kiungo wa zamani wa Liverpool, Momo Sissoko.**




"Nipo kwenye hali nzuri, najisikia kuwa fiti, sasa ninachofanya ni kujenga ufiti wangu, kwa sasa najituma kwa bidii, huku nikiendelea kupona taratibu na naamini ndani ya mwezi nitakuwa fiti kabisa," **mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane.**



"Ni mkali sana [Jose Mourinho] kama kocha, lakini wachezaji wake wengi wanapenda kuzungumza naye kwa upendo, kwa uhakika utavutiwa na mbinu zake na hamasa yake. Hata hivyo, usiposhinda kitu, kocha ndiye mtu anayekuwa dhaifu zaidi kwenye timu na anaweza kufukuzwa wakati wowote," **Michael Ballack ambaye alisajiliwa na Mourinho Chelsea mwaka 2006.**



## Michezo

# WACHEZAJI 15 VINARA WA KADI LIGI KUU BARA



Mshambuliaji wa Azam FC, Obrey Chirwa mmoja kati ya wachezaji vinara wa kadi Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

**Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa Mbao FC, Sylvester Chitembe na Hemed Khoja wa Ndanda FC wamekuwa vinara wa kuonyeshwa kadi nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo kwa sasa imesimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

**Timu za Polisi Tanzania, Azam FC na Ndanda zimeingia mara mbili kwenye 15-bora ya wachezaji wake kuonywa kwa kadi nyingi Ligi Kuu mpaka sasa.**

Kwa mujibu wa takwimu zetu ni kwamba, kati ya wachezaji walioingia 15-bora ya walioonyeshwa kadi nyingi, hakuna mchezaji wa Simba wala wa Yanga. Haya ndiyo majina ya wachezaji waliopigwa kadi nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa...

**1. SYLVESTER CHITEMBE- MBAO FC**

Beki huyu wa Mbao ambaye hucheza beki wa kulia na wakati mwingine beki wa kati, ndiye kinara wa kuzawadiwa kadi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi hivi sasa. Tayari ana kadi saba za njano, lakini vile vile ana kadi nyekundu moja, hivyo kufanya kuwa na jumla ya kadi nane mpaka sasa, ambapo timu yake iko katika hatari ya kushuka daraja.

**2. HEMED KHOJA- NDANDA**

Huyu ni beki wa kati wa Ndanda FC. Hemed Khoja naye ameingia kwenye orodha ya kuwa kinara wa wachezaji waliopata kadi nyingi mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa na kadi saba za njano, lakini kadi nyekundu moja kama mchezaji mwenzake wa Ndanda, Godfrey Malibiche, ambazo alizipata katika harakati za kuwapunguza makali mastraika mbalimbali kwenye ligi hiyo.

**3. PATO NGONYANI- POLISI TANZANIA**

Ni beki wa kati wa Polisi Tanzania ambaye aliwahi kuichezea Yanga. Pato Ngonyani pia ana kadi saba za njano mpaka sasa alizozipata kwenye mechi mbalimbali ambazo timu yake imecheza, akiwa hana kadi nyekundu, na kuwa mmoja wa wachezaji waliopata kadi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

**4. HASSAN MAULID- POLISI TANZANIA**

Huyu pia ni mlinzi wa kati wa timu ya Maafande wa Polisi Tanzania. Kama mwenzake Pato Ngonyani, naye amezawadiwa kadi za njano saba kwenye mechi kadhaa za Ligi Kuu ambazo timu yake imecheza. Yeye hana kadi nyekundu.

**5. GODFREY MALIBICHE- NDANDA FC**

Hucheza nafasi ya beki wa kulia na wakati mwingine beki wa kati kwenye timu ya Ndanda FC. Ameshapigwa kadi saba za njano kwenye Ligi Kuu mpaka sasa akiwa hana kadi nyekundu hata moja, naye akiwa mmoja wa walioongoza kwa kadi nyingi mpaka sasa.

**6. NOVATUS DISMAS- BIASHARA UNITED**

Ni kiungo mkabaji anayeongoza kwa kupata kadi nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Dismas, kiungo mahiri ambaye duru za michezo zinasema kuwa klabu kadhaa zimeshaanza kumnyemelea, ana kadi za njano sita, huku akiwa hana nyekundu.

**7. OBREY CHIRWA- AZAM FC**

Ni mmoja wa mastraika aliyeingia kwenye orodha ya kupata kadi nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Ameshazawadiwa kadi nne za njano ambazo mara nyingi ni aghalabu sana kwa mastraika kupata, kutokana na kwamba wao ndiyo wanaochezewa zaidi rafu.

**8. PAUL NONGA- LIPULI**

Pia huyu naye ni straika, lakini ameingia kwenye orodha ya wachezaji 15 walioonyeshwa kadi nyingi kwenye Ligi Kuu. Nonga mpaka sasa amezawadiwa kadi nne za njano na kuwa mmoja wa mastraika aliopata kadi nyingi msimu huu mpaka sasa.

**9. MICHAEL CHINEDU- ALLIANCE**

Michel Chinedu, straika kutoka nchini Nigeria, kama mgeni mwenzake Mzambia Chirwa, naye ni mmoja kati ya mastraika wachache kwenye Ligi Kuu walioonyeshwa kadi nyingi mpaka sasa. Ana kadi nne za njano, lakini kama mastraika wenzake, hana kadi nyekundu.

**10. ABDULHALIM HUMUD- MTIBWA SUGAR**

Kwa uchezaji wa Humud, ilitegemewa kuwa angeongoza kwa viungo wa ukabaji kupata kadi nyingi zaidi za njano. Lakini mpaka sasa ana kadi nne tu za njano na hana kadi nyekundu.

**11. YAKUBU MOHAMED- AZAM**

Mmoja kati ya mabeki mahiri na wenye uwezo mkubwa kwenye Ligi Kuu nchini Tanzania anayechezea Azam FC, Yakubu Mohamed, naye yumo kwenye orodha ya wachezaji waliopata kadi nyingi kwenye Ligi Kuu. Yeye pia ana kadi nne za njano, lakini mpaka sasa raia huyu wa Ghana hana kadi nyekundu.

**12. DAUD MBWENI- SINGIDA UNITED**

Ni mmoja wa wachezaji waliosajiliwa na Singida United kwenye kipindi cha dirisha dogo, ili kuangalia namna ya kuinusuru kushuka daraja. Daud Mbweni ameshaonyeshwa kadi nne za njano mpaka sasa na kuingia kwenye orodha hii.

**13. MUSSA NAMPAKA- MWADUI**

Ni mchezaji wa nafasi ya kiungo mkabaji na kiungo mshambuliaji kwenye klabu ya Mwadui FC. Naye ameepuka nyekundu lakini akiwa na njano nne.

**14. AUGUSTINO NSATA- MWADUI**

Ni beki wa kati na hucheza kama namba nne. Ni mchezaji wa Mwadui aliyesajiliwa kutoka Ndanda FC. Naye pia ameshapigwa kadi nne za njano na kuingia kwenye orodha ya wachezaji wenye kadi nyingi.

**15. ANTONY AGHATON- LIPULI**

Kwa namna ya kushangaza, huyu ni kipa wa Lipuli FC, lakini naye ameingia kwenye orodha wachezaji walioonyeshwa kadi nyingi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa. Aghaton Mkwando, ameshapigwa kadi nne za njano. Inaonekana kabisa kuwa huyu ni mtaalamu wa kupoteza muda.

**NAJUA WAJUA**



KIPA wa Reims, Predrag Rajkovic ndiye anayeongoza kwa kufanya vizuri zaidi kwenye Ligi Kuu Ufaransa (Ligue 1) msimu huu akiwa ameruhusu mabao 21 ambayo ni machache zaidi ukilinganisha na makipa wengine, lakini hadi sasa amesimama langoni bila kuruhusu bao katika mechi ('clean sheets') 12.

SOKA



Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta (wa pili kulia) akiwa na wachezaji wenzake wa klabu ya Aston Villa. **PICHA: MTANDAO**

# TIMU 3 EPL ZINAZOWEZA KUNUFAIKA NA CORONA

**LONDON,** England

MLIPUKO wa virusi vya corona (covid-19), umeathiri kwa kiasi kikubwa maisha ya kila siku na michezo imeathirika kwa kiwango kikubwa zaidi. Kusimamishwa kwa Ligi Kuu ya England Machi 13, huku ikiwa na uwezekano wa kuendelea Mei 2, mwaka huu kunaonekana kwa kiasi fulani kutazinufaisha baadhi ya klabu.

**Kiukweli kabisa hakuna klabu, shabiki wala mchambuzi wa soka ambaye anapendezwa na hali hii ya kusimamishwa kwa msimu wa ligi wa 2019-20.**

Lakini kwa kile kilichotokea kuna baadhi ya timu zinaweza kunufaika zaidi katika nafasi zilizopo kwenye msimamo wa ligi baada ya kusimamishwa.

Hapa tunaziangalia klabu tatu za Ligi Kuu ya England ambazo zinaweza kunufaika na kusimamishwa kwa ligi hiyo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, hizi hapa...

**#1. LIVERPOOL**

Liverpool kwa sasa wapo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya England wakiongoza kwa tofauti ya pointi 25 dhidi ya wapinzani wao Manchester City, na wiki chache kabla ya kusimamishwa kwa ligi hiyo, ilionekana ni wazi kwamba wanakwenda kushinda taji hilo kwa mara ya kwanza baada ya miaka 30.

Hata hivyo, inaonekana kuna uwezekano msimu huu wa 2019-20 ukafikia mwisho kabisa kwa ligi kutochezwa tena. Kama hilo litatokea maana yake ni kwamba, kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kinaweza kupewa taji hilo.

Lakini kama ligi hiyo itaendelea tena ni kwamba, kikosi hicho cha Klopp kitakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kurudi uwanjani kwa kasi kubwa na pengine kuweza hata kuvunja rekodi ya kufikisha pointi 100 iliyowekwa na Manchester City msimu uliopita.

**#2. TOTTENHAM HOTSPUR**

Kati ya Januari na Februari ilishuhudiwa Tottenham Hotspur ikishinda mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu chini ya kocha Jose Mourinho.

Vipigo kutoka kwa Chelsea na Wolves kwenye Ligi Kuu vilifuata na sare dhidi ya Burnley, huku wakitupwa nje kwenye Kombe la FA na Norwich na kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na RB Leipzig.

Kikosi hicho cha Mourinho kilikuwa kikikabiliwa na majeruhi wengi. Mshambuliaji wake muhimu, Harry Kane alikumbwa na majeruhi na alitarajiwa kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu na hata kutofikiriwa kurudi tena uwanjani msimu huu.

Pia ilikuwa ikikosa huduma ya Moussa Sissoko, Son Heung-min na Steven Bergwijn ambao wote ni majeruhi.

Lakini baada ya kusimamishwa kwa ligi hiyo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona kumetoa nafuu kubwa zaidi kwa Spurs. Kwani sasa wachezaji waliokuwa majeruhi wanaonekana kuwa na nafasi nzuri ya kurudi dimbani mara ligi hiyo itakaporudi tena.

Mourinho sasa atakuwa akitabasamu kuona kwamba wachezaji wake muhimu wanaelekea kupona kabisa kabla ya kuanza tena kwa ligi hiyo na hivyo atakuwa na nafasi nzuri ya kuendelea kupambana na kupigania nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

**#3. ASTON VILLA**

Kabla ya ligi kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Aston Villa walikuwa kwenye hofu kubwa, kwani ilikuwa wazi kwamba kubaki kwenye Ligi Kuu ilikuwa ni ndoto. Kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Leicester kikawaacha kwenye nafasi ya 19 na kuwa kwenye nafasi kubwa zaidi ya kushuka daraja.

Kikosi hicho cha kocha, Dean Smith kilikuwa kwenye hatari kubwa ya kuaga kwenye ligi hiyo baada ya kupanda msimu uliopita.

Lakini kusimamishwa kwa ligi hiyo, sasa ni nafasi nzuri kwa kocha Smith kukifanyia kazi upya kikosi chake ili ligi hiyo ikirudi kiweze kuwa na nafasi nzuri ya kupambana. Pia huu ni wakati mzuri zaidi wa kupumzika kwa wachezaji wake muhimu, Jack Grealish na Tyrone Mings ambao walikuwa wakicheza mara kwa mara.

Hivyo, kipindi hiki ni kizuri zaidi kwa Aston Villa iliyomsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta katika dirisha dogo, kujipanga upya na kurudi kupambana kwa ajili ya kubakia kwenye Ligi Kuu. Na pia wachezaji wake kama John McGinn, Tom Heaton na Wesley Moraes ambao walikuwa majeruhi, sasa wanaelekea kupona na ligi hiyo itakaporudi watakuwa na nafasi nzuri ya kuongeza nguvu kwenye kikosi hicho.

Pia kama ligi hiyo haitaendelea, maana yake ni kwamba, hakuna timu itakayoshuka daraja kutoka Ligi Kuu na hivyo, Aston Villa watakuwa na bahati ya kubakia Ligi Kuu msimu ujao.

KIUNGO wa Manchester City, Kevin De Bruyne ametoa pasi za mwisho 16 hadi sasa msimu huu na yupo kwenye nafasi nzuri ya kuivunja rekodi ya Thierry Henry iliyodumu kwa miaka 17 ya kutoa pasi za mwisho 20 kwa msimu mmoja. Pia ana mabao nane kwa jina lake.



NDANI YA 18

Nipashe
Spotika



KLABU za Ligi Kuu ya soka England na ile ya Hispania, La Liga, hazijawahi kusita kwenye matumizi ya fedha nyingi katika usajili. Klabu hizo zimekuwa zikitumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyake.

Uk. 16&17

# WAKALI WANAOWANIA TUZO MCHEZAJI BORA EPL 2019/20



KEVIN DE BRUYNE

**LONDON,** England

LIGI Kuu nyingi duniani kwa sasa zimesimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19) na moja ya waathirika wakubwa ni mashabiki wa Ligi Kuu ya England. Mashabiki hao sasa watalazimika kusubiri kwa muda mrefu kabla ya ligi hiyo kuanza tena.

Huku baadhi ya wachezaji bora duniani wakiwa wanacheza nchini England, msimu huu umeonekana wa kuvutia kwa viwango binafsi vilivyoonyeshwa na wachezaji wake. Kuanzia magolikipa, walinzi, viungo hadi washambuliaji, wachezaji wa Ligi Kuu ya England wamejiweka kwenye nafasi bora duniani.

Makala haya yakuchambulia wachezaji watatu ambao wana nafasi kubwa zaidi katika mbio za kuwania tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa msimu wa Ligi Kuu ya England, twende sasa...

**#3. JAMIE VARDY**

Jamie Vardy amechomoza katikati ya msitu wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu ya England. Alikuwa nyota bora zaidi wakati Leicester City ikitwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England mwaka 2016. Muingereza huyo msimu huu pia ameibuka na kuwa nyota na sasa ni kinara wa kufunga mabao kwenye ligi hiyo.

Kwa sasa akiwa chini ya kocha, Brendon Rodgers ameendelea kuonyesha ubora wa aina yake kabisa. Pamoja na umri wake wa miaka 33, Vardy kwa sasa anaongoza katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu kwa kufunga mabao 19. Katika nusu ya msimu alifunga mabao nane mfululizo na kujikuta akiweka rekodi ya kufunga mechi 11 mfululizo za Ligi Kuu.

Vardy kwa sasa anaiongoza timu yake kwenye mbio za kuwania kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. Huku zikiwa zimebakia mechi tisa ligi kumalizika, kwa sasa wapo nafasi ya tatu wakiwa wamewazidi Chelsea pointi tano ambao wapo nafasi ya nne.

**#2. SADIO MANE**

Kwa Liverpool, msimu huu ni kama wao, kwani tayari wana pointi 82 na wakifikisha pointi 87 watakuwa mabingwa wa Ligi Kuu ya England. Na itakuwa mara ya kwanza kwa kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kubeba taji hilo kwa kipindi cha miaka 30. Mafanikio ya 'Wekundu' hao yanabebwa na wachezaji watatu kwenye safu yao ya ushambuliaji, wakiongozwa na Sadio Mane. Msimu uliopita akiwa amebeba Kiatu cha Dhahabu kwa pamoja na mchezaji mwenzake, Mohammed Salah na mkali wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, Mane ameendelea kuwa na muendelezo wa kiwango bora zaidi.


Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal tayari amefunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho saba. Muhimu zaidi ni kwamba, mchezaji huyo wa zamani wa Southampton amekuwa na kiwango bora zaidi cha kufunga mabao. Akiwa amefunga bao la kuamua mshindi kwenye mechi dhidi ya Bournemouth, West Ham, Norwich na Aston Villa pa pia dhidi ya washindani wao kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, Manchester City na Leicester City. Mane amekuwa mchezaji ambaye anaibeba Liverpool kwenye nyakati ngumu.

**#1. KEVIN DE BRUYNE**

Baada ya kushinda mataji mara mbili mfululizo huku wakiweka rekodi ya pointi, Manchester City safari hii imekuwa na msimu usioridhisha. Kikosi hicho cha Pep Guardiola ni wazi kwamba kimeshindwa kuonyesha ubora wake na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutetea taji. Hata hivyo, Kevin De Bruyne binafsi amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi. Baada ya mwaka mmoja kusumbuliwa na majeraha yaliyomfanya acheza mechi 19 na kufunga mabao mawili, raia huyo wa Ubelgiji sasa amerudi kwenye kiwango chake kama alivyokuwa msimu wa 2017-18.

De Bruyne ametoa pasi za mwisho kwa mabao 16 msimu huu na yupo kwenye nafasi ya kuvunja rekodi ya Thierry Henry iliyodumu kwa miaka 17 ya kutoa pasi za mwisho 20 kwa msimu mmoja. Pia ana mabao nane kwa jina lake. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 amejiweka mwenyewe kwenye kapu la kuwa mchezaji bora duniani kwa sasa. Kwa uwezo wake wa kutawala nafasi ya kiungo, kunamfanya kuwa mmoja wa wachezaji wenye nafasi kubwa zaidi ya kushinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu ya England, msimu huu.

**USILOLIJUA**



WACHEZAJI wa Juventus na kocha wao Maurizio Sarri wamekubali kutolipwa mishahara yao kwa kipindi cha miezi minne ili kuiokoa klabu hiyo kwa kipindi hiki cha janga la dunia la mapambano ya virusi vya corona (COVID-19, ambapo itaokoa takriban kiasi cha pauni milioni 80.7.





Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei (katikati), akinawa mikono kabla ya kuingia ndani ya Gereza la Ruanda jijini Mbeya, kukagua mrundikano wa wafungwa na mahabusi pamoja na kusikiliza kero zao ikiwa ni mkakati wa jeshi hilo, kwa kushirikiana na vyombo vingine ili kukabiliana na virusi vya corona. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mkakati kupunguza mrundikano wafungwa na mahabusi waanza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya haki jinai likiwamo Jeshi la Magereza, Mahakama na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali mkoani humo limeanza mikakati ya kupunguza mrundikano wa wafungwa na mahabusi katika magereza mbalimbali ili kuepuka madhara ya ugonjwa wa corona.

Vyombo hivyo vilianza kazi hiyo mwishoni mwa wiki ambapo maofisa na watendaji wake walifanya ziara kwenye magereza mbalimbali kwa ajili ya kuangalia hali ya mrundikano na kusikiliza kero zinazowakabilia wafungwa na mahabusi hao.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi baada ya ziara hiyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema waliamua kufanya ziara hiyo kama sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais John Magufuli ya kuwataka kuwapunguza mahabusi.

Alisema katika ziara hiyo walibaini kuwa mkoa huo una wafungwa na mahabusi 1,424 ambao kati yao wafungwa ni 770 na mahabusi ni 654 ambao wanakabiliwa na kesi mbalimbali zikiwamo za mauaji, uhujumu uchumi, unyang'anyi wa kutumia silaha na kesi ndogo ndogo.

Alisema kati ya mahabusi wote waliomo kwenye magereza hayo, 196 wanasubiri vikao vya Mahakama Kuu, 22 wanasubiri Kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), 50 majalada yao yapo katika Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali na wanaosubiri upelelezi wapo 68. "Katika kuhakikisha msongamano wa mahabusi unapungua, nilimshauri Mwakilishi wa Mwendesha Mashtaka wa Serikali wa Mkoa wa Mbeya, Basilius Namkambe, kuwafutia mashtaka mahabusi wenye makosa ya ukorofi, uzembe, shambulio na wizi ambapo alikubali na kuwafutia mashtaka mahabusi saba," alisema Mamanda Matei.

Alisisitiza kuwa taratibu zingine zinaendelea kwa ushirikiano kati ya vyombo hivyo ili kupunguza msongamano.

Alisema katika ziara hiyo pia walisikiliza kero mbalimbali zinazowakabili mahabusi hasa zinazohusiana na Jeshi la Polisi ili kushirikiana kuzitatua mapema.

Aidha, katika hatua nyingine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linamshikilia mtu mmoja ajulikanaye kwa jina la Adelhard Method (37), ambaye ni mfanyabiashara na mkazi wa Mkoa wa Njombe kwa tuhuma za kuwatapeli mali wafanyabiashara kwa kutumia hundi feki za malipo. Alisema mtuhumiwa alikamatwa Machi 24, mwaka huu majira ya mchana mkoani Morogoro ambapo alikuwa kwenye harakati za kutoroka baada ya kufanya matukio mbalimbali nchini ikiwamo mkoani Mbeya.

Alisema mtu huyo alikuwa anaenda kwenye maduka ya wafanyabiashara wanaouza bidhaa za jumla na kufanya nao mazungumzo kama mteja anayehitaji kununua bidhaa na hivyo kuchukua namba zao za simu kisha kuondoka.

"Baada ya muda anapiga simu kwa wafanyabiashara hao akitumia namba za simu ambazo zimesajiliwa na mawakala wasiokuwa waaminifu kwa kutumia vitambulisho vya watu wengine, huwa anaagiza mizigo na kuwashawishi wafanyabiashara hao akiwaomba afanye malipo kwa njia ya hudi," alisema Kamanda Matei na kuongeza.

"Akishatumiwa namba za akaunti anaandaa hundi hewa na kuwatumia kwa njia ya Whatsap, lakini wenye maduka wakienda kuthibitisha hundi hizo na kupata nakala wanabaini kuwa ni hundi hewa na wakati huo anakuwa tayari ameondoka na mzigo," aliongeza. Alisema baada ya kumhoji mtuhumiwa huyo alikiri kuwa huwa anatengeneza hundi hewa ambayo namba yake ya akaunti iliyopo kwenye hundi imefungwa na hivyo upelelezi unaendelea ili kumfikisha mahakamani.

## Rungwe wahimizwa tahadhari ya corona

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MKUU wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Julius Chalya, amewataka wananchi wa wilaya hiyo kuzingatia taratibu zinazoelezwa na wataalamu wa afya ili kukabiliana na ugonjwa wa corona.

Aliyasema hayo alipokuwa ameambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo kukagua utekelezaji wa maelekezo ya serikali ya kuzingatia taratibu za kujikinga na ugonjwa huo ikiwamo kila taasisi kuandaa maji tiririka na sabuni kwa ajili ya watu kunawa.

Kamati hiyo ilifanya ukaguzi huo baada ya kushiriki zoezi la kufanya usafi wa mazingira ambalo hufanyika kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi.

Alisema ugonjwa huo ni hatari na hivyo bila kuzingatia taratibu zinazoelekezwa wanaweza wakajikuta wamepata maambukizi na pengine kupoteza maisha.

"Mnaofuatilia vyombo vya habari mtakuwa mnaona namna ambavyo wenzetu Italia na mataifa mengine ya Ulaya, Asia na baadhi ya mataifa ya Amerika yalivyoathirika, sasa ili tusifikie huko ni kila mmoja wetu kujikinga," alisema Chalya.

Aliwataka wananchi hao kuacha tabia ya kusalimiana mikononi pamoja na kuepuka mikusanyiko isiyokuwa ya lazima ambayo ni hatari kwa maelezo kuwa mikusanyiko hiyo inaweza ikawa chanzo cha kusambaa kwa maambukizi endapo itatokea hata mtu mmoja akawa ameathirika.

Alisema Mkoa wa Mbeya haujawa na maambukizi, lakini akatahadharisha kuwa kutokana na mwingiliano wa watu, ugonjwa huo unaweza ukaingia.

# Rita yaanza kutaifisha mali taasisi 180

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia ofisi ya kabidhi wasii Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita) imeanza kutaifisha mali za taasisi zaidi ya 180 ambazo zimefutiwa usaliji kutokana na kushindwa kujiendesha kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Mbeya na Kabidhi Wasii Mkuu wa Rita, Emmy Hudso, alipokuwa anakabidhi mali zote za iliyokuwa Mbeya Club kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya ili azipangie matumizi mengine yenye tija. Baadhi ya mali za clubu hiyo ambazo alizikabidhi Katibu Tawala ni majengo ambayo yalikuwa hayatumiki tangu ilipoacha kufanya kazi. Emmy alisema taasisi hizo zilifutwa tangu mwaka 2016, lakini mali zake zilikuwa bado zimeachwa kutokana na taratibu za kuzitaifisha kuwa bado kukamilika na kwamba kwa sasa taratibu hizo zimekamilika.

"Kati ya taasisi hizo zilizofutiwa usajili tano zipo mkoani Mbeya na kwa leo tunakabidhi mali za hii Taasisi ya Mbeya Club kwa sababu tayari taratibu zake zimekamilika na tutaendelea na taasisi zingine," alisema Emmy. Alisema baadhi ya mali za taasisi hizo zitakabidhiwa kwa taasisi zingine zenye malengo sawa na zilizofutiwa usajili akitolea mfano wa taasisi ambayo ilikuwa inalea watoto yatima kwamba mali zake zitakabidhiwa kwa taasisi nyingine kama hiyo. Alizitaka taasisi zingine kuendelea kufanya kazi kwa mujibu wa sheria za nchi ili kuepuka rungu la kufutiwa usajili na kwamba ofisi yake pia inahusika na usajili wa vyama vya siasa. Akipokea hati ya makabidhiano ya ofisi za iliyokuwa Mbeya Club, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, alisema menejimeti ya mkoa itakaa na kupanga matumizi ya mali hizo.

Alisema menejimeti hiyo itahakikisha inapanga matumizi ambayo yataiwezesha serikali kuingiza mapato kutokana na mali hizo tofauti na ilivyokuwa awali.

"Kwa sasa hatuwezi kusema tutafanyia kazi gani, lakini baada ya menejimenti kukaa na kujadiliana tutasema tunachotaka kufanyia na lengo letu ni kuhakikisha mali hizi zinakuwa na faida," alisema Dk. Manyatta.

Alisema mkoa huo utaendelea kuzisimamia taasisi zingine ili kuhakikisha zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria za nchi na kwamba kwa zile zitakazokuwa zinakiuka taratibu hatua lazima zichukuliwe.





# Waliojenga kwenye mifereji waonywa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imewataka wafanyabiashara wa masoko kuacha kujenga vibanda vyao juu ya mifereji ya kupitisha maji ili kujiepusha na maji machafu kutuama sokoni.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Masoko wa jiji hilo, James Yuna, alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara wa soko la Sabasaba baada ya kufanya ziara ya kushtukiza akiwa ameambatana na maofisa wa mazingira.

Alisema kujengwa kwa vibanda hivyo juu ya miundombinu ya kupitisha maji ni kuzuia majitaka kutoka nje ya soko na hivyo kusababisha harufu na mazingira ya biashara kuwa chafu.

"Kufanya usafi kwenye mifereji inakuwa mgumu hali ambayo inasababisha maji haya kuzagaa ovyo yakiwa na takataka," alisema.

Aliwataka wafanyabiashara ambao wamejenga juu ya mifereji kwenye masoko yote ndani ya jiji hilo wanajiondoa wenyewe kabla ya kuondolewa kwa nguvu.

"Taratibu za soko zinafahamika na kila mmoja amepata nafasi ya kufanya biashara kisheria ni vyema mkatunza miundombinu ili kuwa na mazingira rafiki," alisema. Alisema mpango wa halmashauri hiyo ni kuona wafanyabiashara wake wanainuka kiuchumi kupitia biashara zao, na siyo kukiuka sheria na taratibu zilizowekwa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, alisema kitendo cha wafanyabiashara kujenga juu ya miundombinu inayopitisha maji inasababisha kushindwa kufanyika kwa usafi kwa wakati.

Alisema mifereji ya maji inatakiwa kuwa wazi muda wote ili kubaini ni wapi kunatakiwa kufanyiwa usafi kwa kuondoa taka ngumu.

"Kitendo cha kujenga juu ya mitaro hii kusababisha kuziba na maji kuzagaa ndani ya soko, tunataka mitaro hii iwe wazi na kwa nia njema na waliojenga waondoe wenyewe," alisema.

Alisema hivi sasa Mkoa wa Dodoma kuna mvua inaendelea kunyesha hivyo hawawezi kuruhusu kuzagaa maji na takataka kila kona kutokana na mifereji kuziba.

"Lazima masoko yetu yawe safi hakuna sababu ya kufanya biashara katika masoko ambayo ni machafu ikumbukwe kuwa kwa sasa mvua zinaendelea lazima mzingatie usafi wa mahali tulipo na tunapofanyia shughuli zetu," alisema.



Wachuuzi wa samaki wabichi katika Soko la Bonanza jijini Dodoma wakisubiri wateja wao, ambao hivi sasa wamekuwa wachache kutokana na hofu ya maambukizi wa virusi vya ugonjwa wa corona. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Mabasi yote kuanza kupulizwa dawa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ameagiza mabasi yote yanayofanya safari zake ndani na nje ya Dodoma ikiwamo daladala kupuliziwa dawa ili kukabiliana na virusi vya ugonjwa wa corona.

Akizungumza na Nipashe jana, Katambi alisema lazima mabasi yote yapuliziwe dawa na kuhakikisha abiria wanaosha mikono yao kabla ya kuingia kwenye gari husika.

"Tunaanza zoezi la kupuliza dawa lengo ni kuendeleza kampeni ya kujikinga na corona," alisema Katambi.

Mkuu alisema dereva wa basi lazima ahakikishe abiria wake wanakuwa salama na kusisitiza watu kutumia vitakasa mikono ili kuua virusi vya ugonjwa huo.

Aliagiza maeneo yote ambayo watu wanaingia ikiwamo baa, maduka na masoko kuweka maji na sabuni ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa huo. "Tabia hii ya usafi iliyojengeka kipindi hiki cha corona iwe mwendelezo wa kila siku ili kusaidia kujikinga na magonjwa ya milipuko kama kipindupindu," alisema.

Kuhusu bei ya vitakasa mikono, Katambi alisema ataendelea kupita kwenye maduka yanayouza kukagua mara kwa mara ili wauzaji wasipandishe bei.

Alisema inapaswa kuuzwa kwa bei elekezi ya serikali ili kila mmoja anunue na kutumia kwa ajili ya kujikinga.

# DC abaini hekari 8 za bangi kupandwa milimani

**Na Mwandishi Wetu,** KONDOA

MKUU wa Wilaya ya Kondoa, Sezaria Makota, amebaini kulimwa kwa hekari nane za bangi juu ya milima ya msitu wa akiba wa Irangi na ametangaza kuwachukulia hatua kali watakaobainika kuhusika kwenye kilimo hicho.

Akizungumza jana baada ya kupanda milima hiyo kwa takribani saa tatu, mkuu huyo alisema amebaini kuwapo na hekari hizo za bangi baada ya kupata taarifa kutoka kwa raia wema.

"Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kondoa kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu nchini (TFS), na serikali ya kijiji cha Mawai na Kata ya Haubi, tulipanga kuja kufanya operesheni kwenye milima ya msitu huu ambao upo mbali sana tumechukua saa tatu na nusu kupanda kutoka kijiji cha Mafai, tumebaini kuna mashamba ya bangi yamepandwa huku juu ya mlima," alisema.

Alieleza kuwa zaidi ya hekari nane zimelimwa bangi kwenye maeneo tofauti ya milima hiyo na zote zitateketezwa.

"Hii ni hatari sana tunashukuru wananchi kwa kutoa ushirikiano wa kutosha, tumekamata pia gunia moja la bangi ambalo lilikuwa limevunwa," alisema.

"Hii operesheni ni endelevu tutahakikisha hakuna kilimo cha bangi Wilaya ya Kondoa na tutakamata wote wanaolima na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria."

Alisema wilaya hiyo imekuwa ikipambana na kilimo cha bangi na kuwaomba wananchi wote wanaojihusisha na kilimo hicho kuacha mara moja.

"Tutahakikisha wale wote wanaojihusisha na kilimo hiki tunawabaini popote walipo," alisisitiza.

Alitoa wito kwa wananchi wa Kijiji cha Mafai, Ntomoko, Kinyasi na Busi kutoa ushirikiano wa kuwakamata wale wote wanaolima bangi.

Naye Kaimu Mhifadhi wa Misitu Kondoa, Elibariki Uisso, alisema wilaya hiyo ndiyo pekee yenye misitu mingi ambayo inahifadhiwa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) ikiwamo msitu wa Irangi.

"Msitu huu ni safu za milima na umezungukwa na vijiji takribani 18, lakini maeneo ya Mafai, Ntomoko na Mwisanga ni ambayo kwa kiasi kikubwa yanaongoza kwa uharibifu wa mazingira, sisi kama TFS tunashukuru Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kudhamiria kukomesha kilimo cha bangi na uharibifu wa mazingira," alisema.

Alisema wakulima wanaolima kilimo cha bangi ndiyo wanachochea kilimo cha mazao mengine kwenye eneo hilo.

"Msitu huu unategemewa na vijiji vingi kwa faida mbalimbali kama upatikanaji wa maji, kama chanzo cha Ntomoko kinachotegemewa na vijiji vingi na kinategemewa pia na wilaya nzima ya Kondoa, hivyo uharibifu huo unachochea chanzo kukauka," alisema.



# Wagonjwa wa corona sasa wafikia watatu

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imethibitisha kuwapo kwa mgonjwa mwingine aliyeambukizwa virusi vya ugonjwa wa corona na kufanya idadi ya wagonjwa hao kufikia watatu.

Akizungumza na waandishi wa habari Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed, alisema mgonjwa huyo ni mwanamke raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 57.

Alisema, mgonjwa huyo aliingia nchini Machi 22, mwaka huu, majira ya saa 2:30 asubuhi na ndege ya Qatar Air akitokea Uingereza. Aidha, alisema mgonjwa huyo ameshapelekwa katika kituo maalum cha kutibu wagonjwa wa corona huko Kidimni Wilaya ya Kati Unguja.

Alisema wagonjwa hao wote wamepata ugonjwa huo kutoka nje ya nchi, na kuwa hadi sasa Tanzania haijazalisha mgonjwa wa corona.

Alieleza kuwa hadi sasa watu 600 waliingia nchini wiki iliyopita kutoka Mombasa nchini Kenya kwa kupitia bandari zisizo rasmi hasa katika Wilaya ya Micheweni Pemba, hivyo aliviomba vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana na wakuu wa mikoa kuhakikisha njia zote zisizo rasmi zinakuwa na askari ili kudhibiti watu wanaoingia kinyume cha utaratibu.

Alisema wananchi wafahamu kuwa hadi sasa nchi 242 duniani zimeshariporti uwapo wa virusi hivyo, huku bara la Afrika nchi 43 zimeripoti uwapo wa kirusi hicho na Afrika Mashariki nchi nne zimebainisha kuwa na ugonjwa huo zikiwamo Kenya, Uganda, Rwanda na Tanzania.

Hamad alimtaka Mufti Mkuu wa Zanzibar kutafuta njia ya kuendelea kuelimisha waumini wa dini ya kiislamu wanaotumia nyumba za ibada kuzingatia suala la masafa baina ya mtu na mtu kwa kuwa upo uwezekano wa kuambukiza maradhi hayo.

Aidha, aliwataka wananchi kuendelea kutii maagizo yaliyotolewa na serikali ikiwamo kuacha mikusanyiko isiyo ya lazima na pale mtu anapotoka nje ya nchi kuchukua tahadhari mwenyewe ili kuwakinga na wengine.

"Mgonjwa mmoja asiyechukua tahadhari na kuwaonea huruma Wazanzibari na Watanzania ya kutoa taarifa mapema akachunguzwa na badala ya kwenda kujumuika na wananchi kwani athari yake ni kubwa sana ikiwamo kuongeza mzigo wa kuwachunguza wengine," alisema.

Aliwasisitiza wananchi kupunguza mambo yasiyokuwa ya lazima kwa kuwa hata nchi zenye wataalamu na vifaa vya kutosha kama Italia na Marekani zimeshindwa.



Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu Zanzibar na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, jana, alifanya ziara maalumu kwenye jimbo hilo kutoa elimu ya kujihadhari na maambukizi ya virusi vya corona na kutoa msaada wa kitanda maalumu kwenye kambi ya kuhudumia wenye maambukizi ya virusi hivyo, pamoja ndoo na sabuni kwenye maskani, masoko na migahawa. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Wazee watakiwa kuchukua hadhari corona

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

JUMUIYA ya Waastaafu na Wazee Zanzibar (JUWAZA), imewataka wazee kuwa na tahadhari juu ya kukabiliana na mlipuko wa virusi vya corona.

Hayo yalielezwa na Katibu wa Jumuiya hiyo, Salama Kombo Ahmed, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar.

Alisema kinga za mwili za wazee ni ndogo, hivyo ni rahisi kupata maambukizi ya maradhi hayo, hivyo katika kipindi hiki wanahitaji kuwa na tahadhari zaidi ili kujiepusha na maambukizi.

Alisema licha ya serikali kutoa elimu kwa jamii, lakini jitihada zaidi zinahitajika katika kuwafikia wazee wote wa mijini na vijijini ili kuwaelimisha juu ya kujikinga na maradhi hayo. "JUWAZA tumeamua kutumia fursa hii kuwakumbusha na kuwaelimisha wazee juu ya hali halisi iliyopo hivi sasa nchini kwani wengi wao wenye umri kuanzia miaka 60 na kuendelea hawafahamu kinachoendelea nchini," alisema.

Akiwataja wazee ambao wapo hatarini zaidi kupata maradhi hayo ni wenye magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo kisukari, magonjwa ya moyo, saratani na wanaopata matibabu ya mionzi.

Aliitaka jamii inayoishi na wazee hao kuchukua juhudi za makusudi katika kipindi hiki kwa kuwasimamia na kuwaangalia usalama wao pamoja na kuwaosha mikono na kuchukua tahadhari zote ili kuwakinga na magonjwa hayo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Masururu Saad Feroudh, aliwataka wazee hao na jamii kujikita zaidi katika kufanya ibada na visomo kumwomba Mungu ili kuyaondosha maradhi hayo.

# Mjini Magharibi sasa waonywa mikusanyiko

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Mgharibi Unguja, Hassan Khatib Hassan, amewataka wananchi wa mkoa huo kuepuka mikusanyiko isiyokuwa ya lazima na kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Akizungumza baada ya kufanya ziara katika soko la Mwanakwerekwe na Darajani, Hassan alisema baadhi ya wananchi wamekuwa na tabia ya kukaa katika makundi bila ya shughuli maalum na kukiuka maagizo na maelekezo ya serikali ili kukabiliana na maradhi hayo.

Alisema endapo wananchi wataendelea kukaidi maelekezo yaliyotolewa na serikali, serikali ya Mkoa itawachukulia hatua wale wote watakaobainika kudharau maagizo hayo, na kuwaweka kizuizini kwa muda wa siku 14 na kujihudumia wao wenyewe.

Aidha, Mkuu wa Mkoa huyo alisema serikali haina dhamira ya kuwawanyanyasa wananchi wake, lakini wakati umefika sasa kwa wananchi kufuata maelekezo na elimu inayotolewa na wataaalamu wa afya ili kujinusuru na janga hilo kubwa la maradhi ya corona ambalo limeikumba na kuiathiri dunia.

Akizungumzia kuhusu hali ya mazingira katika masoko ya mkoa huo, aliuagiza uongozi wa serikali ya Wilaya ya Mjini kushirikiana kwa karibu na Manispaa ya Mjini katika kuwasimamia viongozi na watendaji wa soko la Mwanakwerekwe ili kuona linakuwa katika mazingira mazuri.

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa mkoa aliupongeza uongozi wa soko la Darajani na soko la mboga Mombasa kwa hatua nzuri wanazozichukua katika kuyaimarisha masoko hayo kwa utoaji wa huduma na usafi wa mazingira.

Aidha, alitaka jumuiya ya wafanyabiashara wa soko la Mwanakwerekwe kukaa pamoja na viongozi wa soko kuchukua hatua za haraka katika kuimarisha usafi na kuacha tabia ya kufanya biashara katika maeneo ya chini.

Kwa upande wao, wafanyabiashara wa soko hilo walimhakikishia mkuu wa mkoa huyo kuwa watafuata maagizo yote yanayotolewa na serikali katika hatua za kudhibiti ongezeko la maambukizi ya virusi vya corona.

HABARI KITAIFA

# Kibano kwa h/shauri kulipa kodi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, ameziagiza halmashauri zote nchini, kuhakikisha maeneo yao ya biashara yanapimwa na kupatiwa hati, ili kulipa kodi ya serikali.

Mabula alitoa agizo hilo wakati akizungumza na wakurugenzi wa halmashauri zote, maofisa mipango miji na wafanyakazi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) mkoa wa Kagera, na kuwa halmashauri nyingi hazitaki kupima kwa makusudi ili zikwepe kodi ya serikali, wakati zinafanya biashara.

"Lakini halmashauri nyingi hazitaki kupima makusudi ili zikwepe kodi ya serikali, sasa tunapokwenda kwa wamiliki wa kawaida kudai lazima na sisi tujiangalie tunafanya nini...kwa hiyo naagiza maeneo yenu yote yapimwe na kupewa hati na yaanze kulipiwa kodi," alisema.

Aidha, alisema hajaridhishwa na hali ya makusanyo ya mkoa wa Kagera na kuwa hadi sasa kodi iliyokwishakusanywa ni asilimia 23.

"Ukiangalia kasi ya Mheshimiwa Rais John Magufuli ya utekelezaji wa miradi kitaifa sehemu kubwa inategemea pesa za ndani na ardhi ni sekta ambayo kama inasimamiwa vizuri na watu wanajituma katika kusimamia mapato, inaweza kuongeza pato la serikali kwa kiwango kikubwa," alisema.

Alisema kwa mkoa mkubwa kama Kagera wenye halmashauri nane na wilaya saba, unapokusanya asilimia 23 ndani ya miezi tisa ni changamoto inayohitaji kusimamiwa, na kuwa amezungumza na mkuu wa mkoa Brigedia Jenerali Marco Gaguti, na kumweleza aongeze kasi ili kuboresha makusanyo ya sekta ya ardhi.

"Lakini jambo jingine ni katika suala la ufuatiliaji madeni wako taratibu sana, hawafanyi nilichoelekeza, kwa sababu unapopeleka ilani kwa mteja yeyote ndani ya siku 14 anatakiwa kuwa amelipa kwa hiari, au akishindwa anapaswa kupelekwa kwenye baraza... sasa kuna ilani zilipelekwa tangu mwaka jana, lakini mpaka leo hatua hazijachukuliwa," alisema.

Alisema kuwa haina maana kupeleka ilani halafu usifuatilie na kuwa amewasisitiza kubadilika na kwa kuwa wanafungua ofisi za mikoa, watumie fursa hiyo kuhakikisha kazi ya ufuatiliaji madeni inafanyika.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi katika mikoa ya Mwanza na Kagera, Biswalo Makwasa, alisema katika malengo ya jumla ya makusanyo kodi, mkoa wa Kagera ulipaswa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 3.5 katika mwaka wa fedha 2019/2020. "Hadi sasa umekwishakusanya shilingi milioni 801, dalili hiii siyo nzuri, lakini bado ninaamini kwamba wakiongeza jitihada kufikia Juni 30 mwaka huu watakuwa wamefikia malengo," alisema Makwasa.

Naye Meneja wa NHC mkoani wa Kagera, Benit Masika, alisema malengo waliyopangiwa ni kukusanya zaidi ya Sh. milioni 982.6 na kuwa hadi Februari 2020 wamekwisha kusanya zaidi ya Sh. milioni 763.8 na kuwa wana matarajio ya kukamilisha lengo.



Mfanyabiashara wa soksi katika kituo cha mabasi ya kwenda mikoani Ubungo jijini Dar es Salaam akitafuta wateja juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waliokopa mamilioni NSSF bila kurejesha nyumba zao kuuzwa

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) wilayani Kahama mkoani Shinyanga, linadai kiasi cha Sh. milioni 850 kutoka kwenye Chama cha Ushirika Ibuka Saccos.

Chama hiki kilikopeshwa fedha hizo na shirika hilo tangu mwaka 2017, hivyo limeanza kufuatilia nyumba zikizowekwa kama dhamana.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya waliokopa kukimbia, hivyo nyumba hizo pamoja na rasilimali zingine vimeanza kuuzwa kufidia madeni hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, aliyasema hayo kwenye mkutano mkuu wa nane na kuwakutanisha wajumbe wa Ibuka Multipurpose Cooperative Society Ltd, huku akiwataka kulipa fedha hizo haraka ili wengine waweze kukopeshwa.

Macha alieleza akusikitishwa na kitendo hicho baada ya kuelezwa chama kudaiwa kiasi hicho cha fedha ambacho kilikopeshwa tangu mwaka 2017, na kuwataka walipe deni hilo bila hivyo nyumba zao zitapigwa mnada.

"Hakuna sababu ya wananchi kuendelea kuteseka na ushirika usio salama, nasisitiza madeni mliokopa NSSF mlipe...mkae mjadiliane kwenye mkutano huu, kwani tutaanza kufuatilia nyumba mlizoweka dhamana mkakopesheka," alisema Macha.

Macha alisema fedha hizo kwa utaratibu uliopo ni kukopa na kurejesha kwa wakati, lakini sasa ni miaka mitatu tangu walipokopa, hawajarejesha.

Mrajisi Msaidizi wa Mkoa wa Shinyanga, Winston Nsemwa, aliwataka wasivunje ushirika huo bali wajadili masuala ya maendeleo na mustakabali mzima wa ushirika, huku akiwataka viongozi kuwa waadilifu.

Naye Meneja wa Chama cha Ushirika Ibuka, Mkama Kadidi, alisema fedha hizo zilikopwa na wanachama 74 wa Ibuka Saccos na waliorejesha mpaka sasa ni wanachama watano ambao wamemaliza mkopo wao.

Meneja wa NSSF Kahama, Aisha Nyemba, alithibitisha kuidai Ibuka Saccos Sh. milioni 850, ambazo walikopeshwa tangu 2017 bila kurejesha.

# Walia kuadimika kwa koki za plastiki

**Neema Sawaka,** KAHAMA

BAADHI ya wafanyabiashara wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamelalamikia kuadimika kwa koki za plastiki za mabomba wilayani humo.

Wamesema hali hiyo inatokana na kulanguliwa kwa wingi na kusafirishwa kwenda jijini Dar es Salaam, huku ndoo moja bado ikiuzwa kwa Sh. 30,000.

Kuwapo kwa hofu ya kuenea kwa ugonjwa wa corona kumeelezwa kuwa sababu ya kupanda kwa bei ya koki za plastiki kutokana na mahitaji zaidi.

Hayo yalisemwa jana na mfanyabiashara mwenye duka la vifaa hivyo mjini Kahama, ambaye ni mhasibu wa kamati ya maendeleo ya Kanisa la AIC Pastorate ya Nyihogo, Charles Machali, alisema wafanyabiashara kutoka jijini Dar es Salaam walikuwa kuzilangua zote madukani kwa bei ya jumla.

Machali alisema wakazi wa Kahama wameanza kuhangaika kutafuta pa kuzipata kutokana na uhaba huo.

Machali alisema kuwa kabla ya virusi vya corona, koki hazikuwa na soko na zilikuwa zinakaa madukani muda mrefu.

"Soko limekuwa kubwa kwa ghafla, mahitaji ni mengi kutokana na wananchi kujikinga na virusi vya corona kwa kunawa mikono," alisema Machali.

Nao wajasiriamali wadogo mjini Kahama, Musa Peter na Scolastika Amos walieleza kukaguliwa kwa kila mlango na maofisa afya wa halmashauri kwa kusisitiza kila mmoja awe ndoo ya kunawia, lakini changamoto wanayoeleza kuadimika kwa mabomba ya plastiki.

Peter alisema bomba za plastiki bei yake ni nafuu tofauti na za chuma zenye kufungulia hata kwa kiwiko zina gharama kubwa ambapo doo moja kuuzwa kwa Sh. 30,000, hivyo gharama ni kubwa hawawezi kuimudu.

## Vifo vya corona Ulaya, Marekani vyafikia 20,000

**WASHINGTON,** Marekani

IDADI ya vifo kutokana na virusi vya corona imepanda na kufikia watu 20,000 barani Ulaya, huku Italia na Uhispania kila moja ikiripoti vifo vya zaidi ya watu 800 katika siku moja.

Nchini Marekani, idadi ya vifo imefikia zaidi ya watu 2,000 huku idadi ya maambukizi ikifikia 120,000.

Idadi ya watu waliofariki duniani kutokana na ugonjwa huo imefikia 30,000 na maofisa katika baadhi ya nchi wanasema hali itaendelea kuwa mbaya katika siku zijazo.

Lakini katika mji wa Wuhan nchini China ambao virusi hivyo vilianzia, maofisa wameanza kuchukua hatua za kurejesha hali ya kawaida, kwa kufungua sehemu mji huo baada muda wa miezi miwili ya kufunga kabisa mji huo wenye idadi ya watu milioni 11.

Theluthi moja ya idadi ya watu duniani wamefungiwa majumbani wakati virusi hivyo vikiendelea kuvuruga kila muhimili wa jamii kwa kusababisha ukosefu wa ajira, kuelemea mifumo ya huduma za afya na kuziweka hatarini bajeti za serikali katika miaka inayokuja. **DW**

## Wakazi Kinshasa wazuiwa kutoka nje wiki tatu

**KINSHASA,** DRC

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imefunga mji wa Kinshasa kwa muda wa wiki tatu kuzuia maambukizi katika miji mingine, agizo lililoanza kutekelezwa kuanzia juzi.

Uamuzi wa marufuku hiyo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Gavana wa Mkoa wa Kinshasa, Gentiny Ngobila. Mkoa wa Kinshasa ni kitovu cha ugonjwa wa virusi vya corona ambao tayari umesababisha vifo vya watu wanne kati ya wagonjwa 54 walioambukizwa virusi vya ugonjwa huo.

Wakati huohuo, DRC imethibitisha kuwaweka watu 2,000 karantini ambao wamehusiana na wagonjwa hao wa Covid-19. Mmoja kati ya wagonjwa hao ni kutoka Kaskazini mwa Mkoa wa Kivu Kaskazini, Mashariki mwa DRC.

Raia wameonekana wakilalamikia hatua hiyo ambayo serikali imeichukua kutokana na hali ya maisha ya wengi wanategemea kipato cha dola moja au chini ya hapo.

Hata hivyo, Gavana Gentiny Ngobila amebaini kwamba hali hiyo inatia wasiwasi na ameamua kufunga mji wa Kinshasa kwa muda wa wiki tatu.

“Maofisa wa utawala wa umma pekee pamoja na wafanyakazi katika sekta ya afya ndio wataruhusiwa kwenda kazini,” alisema Gavana Ngobila.

Wakati huohuo, serikali ya DRC imewaonya wafanyabiashara kutopandisha gharama ya vitu wakati huu ambao hali si nzuri. **RFI**

# Waliokatazwa kutoka nje Rwanda wapewa vyakula

**KIGALI,** Rwanda

**Mpango wa ugawaji chakula umeanza katika Mji Mkuu Kigali, lakini maofisa wanasema utaendelea katika miji mingine midogo nchini humo.**

FAMILIA zilizoathiriwa na sheria ya kukaa nyumbani nchini Rwanda zimeanza kupokea msaada wa chakula kutoka serikalini.

Familia hizo ni zile zilizoathiriwa na agizo la kukaa nyumbani lililowekwa nchini humo ili kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona.

Idadi ya visa vya maambukizi ya ugonjwa huo imefikia watu 60 huku wengine mamia wakiendelea kuchunguzwa baada ya kukutwa na dalili za awali.

Jumamosi pekee Rwanda ilitangaza visa sita vipya vya ugonjwa wa virusi vya corona. Hali hiyo inalifanya taifa la Rwanda kuwa na idadi kubwa zaidi ya visa vya ugonjwa huo vilivyothibitishwa kuliko mataifa mengine ya Afrika Mashariki.

Hatua ya ugawaji wa chakula ilianza juzi baada ya Rais Paul Kagame kuelezea katika hotuba yake kuwa serikali yake itawasaidia Wanyarwanda wanaoathiriwa zaidi katika kipindi cha agizo la kukaa nyumbani.

Wafanyakazi wanategemea malipo ya kila siku kwa ajili ya kuishi katika maeneo ya mjini ndiyo walioathiriwa zaidi kutokana na kusimamishwa kwa shughuli wanazozifanya.

Mpango wa ugawaji chakula umeanza katika Mji Mkuu Kigali, lakini maofisa wanasema utaendelea katika miji mingine midogo nchini humo.

Chakula kinachotolewa kimetoka katika hifadhi ya taifa ya vyakula vya nafaka inayosimamiwa na Wizara ya Mifugo.

Mwanzoni mwa wiki hii, Rwanda ilitangaza kufunga mipaka yote ya nchi hiyo na watu kuamrishwa kusalia majumbani katika juhudi za kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona.

Hatua zingine zilizochukuliwa ni pamoja na watumishi wote wa serikali na sekta binafsi kufanyia kazi nyumbani na safari za kwenda mikoani kusitishwa kwa wiki mbili kukiwa na uwezekano wa muda huo kuongezwa.

Vilabu vya pombe na maduka yasiyo ya chakula pia yamefungwa huku usafiri wa bodaboda ukisitishwa.

Hatua hiyo ilichukuliwa siku moja baada ya Wizara ya Afya ya Rwanda Jumamosi kutangaza kuwa watu wengine sita wameambukizwa virusi vya corona miongoni mwao mtoto mchanga wa miezi 10.

Maambukizi hayo yanaifanya Rwanda kuwa na idadi ya matukio 17 ya maambukizi ya virusi vya corona. **BBC**



Mmoja wa wakazi wa Jiji la Kigali Rwanda akipokea msaada wa chakula kutoka kwa maofisa wa serikali baada ya kutangazwa zuio la wananchi kutotoka nje. **PICHA: REUTERS**

# Boko Haram waua wanajeshi 150 Chad, Nigeria ndani ya siku tano

**LAGOS,** Nigeria

KUNDI la kigaidi la Boko Haram limewaua takribani wanajeshi 150 katika mataifa ya Chad na Nigeria ndani ya kipindi cha siku tano zilizopita.

Kwa mujibu wa Rais wa Chad, Idriss Deby wanamgambo hao wa Boko Haram waliwaua wanajeshi 92 wa nchi yake na kuwajeruhi wengine 47 katika mashambulizi mabaya kabisa dhidi ya jeshi Jumatatu iliyopita.

Taarifa ya Rais Deby ilitolewa Juzi jioni, wakati kiongozi huyo ambaye ni mwanajeshi alipotembelea kisiwa cha Boma kwenye Ziwa Chad, magharibi mwa nchi hiyo, ambako mashambulizi hayo yalifanyika.

Muungano wa kijeshi wa mataifa ya Chad, Niger na Nigeria umeweka kambi yake huko kupambana na uasi wa Boko Haram, ambao umesambaa kwenye mataifa kadhaa ya magharibi mwa Afrika na ukanda wa Sahel.

“Nimewahi kushiriki kwenye operesheni kadhaa za kijeshi, lakini haijawahi kutokea kwenye historia yetu kupoteza wanajeshi wengi kama hawa kwa wakati mmoja,” Deby aliwaambia waandishi wa habari.

Huko kaskazini mwa Nigeria nako, wanamgambo wa Boko Haram wanaripotiwa kuwaua wanajeshi wengine 50 wa Nigeria katika Jimbo la Yobe, kwa mujibu wa duru za kijeshi.

Msemaji wa Jeshi la Nigeria, Meja Jenerali John Enenche, aliliambia Shirika la Habari la AP kwamba jeshi lake limepoteza watu wengi katika kile alichokiita bahati mbaya, ingawa alikataa kutaja idadi kamili ya wanajeshi waliouawa.

Jeshi hilo lilivamiwa wakati likijiandaa na kuanzisha mashambulizi dhidi ya Boko Haram, kwa mujibu wa ofisa mwingine wa ngazi za juu wa jeshi, ambaye anafahamu operesheni hiyo.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, wanajeshi walikabiliana na wanamgambo hao kwa muda mchache, lakini baadaye walilazimika kukimbia kunusuru maisha yao, kabla ya kurejea tena kupambana na kushambuliwa kwenye kijiji kimoja kiitwacho Gorge. **DW**

HABARI KITAIFA

# Komu kutimkia kwa Mbatia, Chadema yamjibu

**Na Mwandishi wetu**

MBUNGE wa Moshi Vijijini, Anthony Komu, amesema kuwa ataondoka Chadema atakapomaliza ubunge wake, huku akiweka bayana kuwa hatagombea ubunge kupitia chama hicho bali NCCR-Mageuzi.

Aidha, amesema iwapo atatakiwa kugombea ubunge atafanya hivyo kupitia NCCR-Mageuzi katika jimbo lolote atakalotakiwa kufanya hivyo.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni, alisema msimamo huo utasaidia kupunguza maneno yanayoendelea, na kwamba uamuzi huo unakipa nafasi chama fursa ya kujiandaa kwa ajili ya uchaguzi wa 2020.

"Huu ni utamaduni mzuri ambao ni vyema ukaigwa, ni utamaduni mpya uigwe na waliyo na mipango ya mifukoni tofauti na vyama vingine, nimeiga utamaduni wa Wakenya ambao husema bayana, ni matumaini yangu chama changu kitachukua suala hili kwa mtazamo chanya na kuzingatia misingi iliyopo kwenye katiba na sera zetu," alisema.

Alisema kwa muda mrefu amekuwa kwenye mgogoro na chama chake kwa kuwa wanatofautiana katika uendeshaji wa chama hasa kimuundo, kupangana katika nafasi mbalimbali ndani ya chama na vipaumbele katika kushika dola.

"Kwa muda mrefu nimenyamaza ili wanaofahamu ukweli wanisemee, bahati mbaya waliojaribu kunisemea walituhumiwa, vita ya maneno ikawa kubwa, yote haya kwa faida ya nani na kwanini tumekuwa watunzi wa riwaya na wapiga ramli," alisema.

Aidha, alikiri kuwa wamekuwa wakitofautiana na kwamba kuwa na mtizamo tofauti imeonekana ni uhasi, na hivyo kushindwa kutumia fursa na uwezo alionao katika kukiimarisha chama.

"Dhana nzima ya kupendana na kuamianiana imeondoka, badala yake tunatuhumiana, tunabaguana na kujengeana uadui wenyewe... hili limeongezeka baada ya uchaguzi mkuu wa chama ambao umeacha majeraha makubwa," alisema.

"Uamuzi huu si wakukurupuka si wa kibabe, nimeshirikisha watu wengi ninaowaamini wana mapenzi mema na nchi, ambao wamechangia mafanikio niliyoyapata katika harakati zangu za kisiasa...naamini chama kitaheshimu uamuzi wangu," alisema.

Alisema hakuingia kwenye siasa kufuata mtu au kufuata maslahi binafsi bali maslahi mapana ya nchi na kwamba walijinyima ikiwamo kuacha kuajiriwa kwa kuwa wakati huo hakukua na shida ya ajira.

**AOMBA MSAMAHA WANA NCCR**

Aidha, alisema kaamua kurudi NCCR -Mageuzi kutokana na itikadi yao ya utu, utulivu na ukomavu uliopo baada ya kupitia matatizo makubwa kuanzia mwaka 1995 kikiwa chama kikuu cha upinzania nchini ambacho kilipoteza kila kitu mwaka 2000.

Alisema sababu nyingine ni kauli ya Mwenyekiti, James Mbatia, kuwaomba msamaha na kuwaomba waliokwazwa na chama hicho warejee ili kukijenga upya chama, na kwamba kauli hiyo imemgusa na kwamba ni ya kiungwana na yenye ukomavu wa hali ya juu.

"Naungana na Mbatia kuwaomba radhi wote ambao mienendo yangu katika harakati hizi nimewahi kuwakwaza, nilikuwa NCCR nikaondoka kwa hiari yangu nikaenda Chadema na niliwashawishi Mwanasheria Mabere Marando, Prof. Baregu na Mbunge wa Rombo Joseph Selasini niliwapa kadi mwenyewe... niwaombe waliobaki NCCR wakati ukifika wanipokee tena ninayo ndoto ya kujenga upinzani imara na endelevu," alisema.

**CHADEMA YAMJIBU**

Akijibu kauli hizo, Msemaji wa Chadema, Tumaini Makene, alisema mbunge huyo ameonyesha ubinafsi wa kiwango cha kutisha katikati ya masuala mazito na muhimu yanayogusa wananchi anaopaswa kuwawakilisha na kuwa msemaji wao.

"Komu kaamua kutangaza kuwa yupo Chadema kwa sababu ya kusubiri mafao ya ubunge na posho za bunge la bajeti, kwa sababu atajiondoa kwenye chama baada ya ubunge wake kumalizika," alisema.

"Hayupo kwenye chama kwa sababu ya itikadi, imani, falsafa au misimamo ya chama, bali yuko kwa sababu analazimika kusubiri mafao ya kiinua mgongo. Ni ajabu sana mtu wa kiwango cha Komu kutoa kauli inayomuanika na kumweka wazi kuwa anasukumwa na tumbo lake," ilisema taarifa hiyo.




Mfamasia Mkuu wa Serikali, Daudi Msasi (katikati), akitakasa mikono yake katika moja ya vifaa 100 vya kutakasia mikono vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 30 vilivyotolewa na Benki ya Biashara ya DCB, vitakavyowekwa katika vituo mbalimbali vya daladala na mwendokasi jijini Dar es Salaam, ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na ugonjwa hatari wa homa ya mapafu wa corona (Covid-19). Hafla hiyo ilifanyika katika ofisi za Wizara ya Afya jijini Dar es Salaam jana, kushoto ni Mkurugenzi wa Masoko na Mawasiliano wa DCB, Rahma Ngassa na kulia ni Mkurugenzi wa Msaidizi wa Afya Mazingira wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Khalid Massa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Shein aongoza mazishi ya Haji Faki

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, jana aliongoza mazishi ya Waziri Kiongozi mstaafu, Brigedia Jenerali Ramadhan Haji Faki, yaliyofanyika kijijini kwao Mkwajuni, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa, dini na serikali pamoja na wananchi, ndugu na jamaa walihudhuria katika mazishi hayo akiwamo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa ambaye alimwakilisha Rais John Magufuli.

Viongozi wengine waliohudhuria ni Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, Brigedia Jenerali wa Brigedi ya Nyuki Zanzibar Fadhil Omar Nondo, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Said Hassan Said, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdalla Juma Mabodi, Mawaziri na viongozi wengine wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mapema Dk. Shein aliungana na viongozi wa dini, vyama vya siasa na serikali, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi katika sala ya kumsalia marehemu Waziri Kiongozi mstaafu Faki katika Msikiti wa Mushawar, Mwembeshauri, Mjini Unguja sala iliyoongozwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kahbi.

Mazishi ya Waziri Kiongozi mstaafu Brigedia Jenerali Mstaafu Ramadhan Haji Faki yalifanyika kwa taratibu zote za kidini na kijeshi ikiwamo kutolewa salamu za heshima, salamu za kijeshi pamoja na kupigia mizinga 17, zoezi lililoongozwa na gwaride chini ya kiongozi wake Himid Alawi Nguzo.

Akisoma wasifu wa marehemu, Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mohammed Aboud Mohammed, alisema kuwa alizaliwa mwaka 1930 katika Kijiji cha Mkwajuni, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

## Wavutaji sigara wanaosumbua wapewa angalizo

**Na Said Hamdani,** LINDI

SERIKALI mkoani Lindi imewataka watu wanaovuta sigara kwenye mikusanyiko, kutafuta utaratibu utakaoepusha kuleta usumbufu, ikiwamo kuambukizana maradhi yanayotokana na uvutaji sigara.

Angalizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa huo, Godfrey Zambi, alipokuwa anazungumza kwa nyakati tofauti na wafanyabiashara na wananchi wa mji wa Lindi wakati wa ziara yake ya kukagua na kuhimiza usafi na namna ya kujikinga na ugonjwa hatari wa corona.

Zambi alitoa maelekezo hayo kutokana na baadhi ya wafanyabiashara wa soko kuu la vyakula kulalamikia kitendo cha baadhi ya wenzao, wakiwamo wabeba mizigo kuvuta sigara kwenye mkusanyiko wa watu, jambo ambalo limekuwa kero kwao na wengine wanaofika kupata huduma.

Akizungumza na wafanyabiashara na wananchi waliojitokeza kupata huduma kwenye soko kuu la vyakula, samaki na mboga, Zambi alisema serikali imeshakataza uvutaji wa sigara kwenye mikusanyiko ya watu.

Zambi alisema mtu yeyote anayehitaji kuvuta sigara ni vizuri wakatafuta eneo wavute, badala ya kutumia mikusanyiko ili kuepusha usumbufu kwa wengine ambao hawahusiki na uvutaji huo.

Aidha, ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kusimamia usafi kwa karibu zaidi ikiwamo kuondoa tela la kuhifadhia taka mara tu linapokuwa limejaa badala ya kuwapo kwa muda mrefu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** Ninauza nyumba ya vyumba vinne vya kulala, kimoja ni master self contained. Ina vyumba vitano vya nyuma kimoja ni self contained, choo, bafu na jiko. Nyumba iko Ntyuka Dodoma karibu na shule ya sekondari Ntyuka. Nyumba iko kwenye kiwanja cha ukubwa wa SQM 2590. Ni nyumba nzuri sana kwa makazi na kupangisha. Kwa maelezo zaidi piga simu no. 0699-210258


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu:**




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# CHELSEA KUTANUA UWANJA WAO WA STAMFORD BRIDGE

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea imethibitisha kwamba, wanafikiria mpango wa kuendeleza Uwanja wa Stamford Bridge, ambapo ruhusa yao ya sasa inamalizika Machi 31, mwaka huu.

Klabu hiyo ilipewa ruhusa ya kutanua Uwanja wa Stamford Bridge ili uwe na uwezo wa kuchukua watazamaji 60,000, ingawa taarifa zinasema kwamba, mradi huo ulisimama.

Hata hivyo, tangu walipopewa ruhusu ya upanuzi huo Machi mwaka 2017, hakuna kazi yoyote iliyofanyika.

Lakini sasa imethibitishwa na gazeti la Daily Mail kwamba, Chelsea wanafikiria kuendelea na mpango wa kutanua uwanjani huo, ingawa ruhusa yao inamalizika kesho, Jumanne.

"Tuna imani kubwa kwa mashabiki wetu na washikadau, hasa Kampuni ya Hammersmith & Fulham Council, kwa kuwa wavumilivu na kuelewa nini kinachoendelea," ilisema taarifa ya klabu hiyo iliyowekwa kwenye tovuti ya klabu hiyo.

"Tutaendelea kufikiria kuhusu mpango wetu wa uwanja mpya, kwani pia ni jambo la kuimarika kwa uchumi."

# Coutinho apigania kurudi England

**MUNICH,** Ujerumani

WAWAKILISHI wa mshambuliaji wa Barcelona, Philipe Coutinho wameripotiwa kuangalia uwezekano wa mchezaji huyo kurudi tena kwenye Ligi Kuu ya England.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, wawakilishi hao wameonekana kusitisha mazungumzo na kuzitupilia mbali ofa za klabu za Paris Saint-Germain na Inter Milan ambazo zilikuwa zinamuwania kwa udi na uvumba.

Msimu uliopita klabu yake ya Barcelona ilifikia makubaliano ya kumpeleka kwa mkopo mchezaji huyo kule Ujerumani kuichezea klabu ya Bayern Munich. Lakini, kwenye mkataba huo kulikuwa na kipengele cha kumnunua kabisa na kama miamba hiyo ingehitaji kufanya hivyo, ingewalazimu kutoa euro milioni 120.

Hata hivyo, Coutinho hajaonyesha kiwango cha kuishawishi Bayern kutoa kiasi hicho cha fedha ili kumsajili, hii ni kutokana na kuwa na kiwango cha chini. Hivyo Bayern hawajaonyesha dhamira ya kumchukua.

Coutinho anahitaji kurudi katika Ligi Kuu mahala ambapo alicheza Liverpool kwa mafanikio.





# *Mustafi: Sijui hatima yangu hapa Arsenal*

**LONDON,** England

SHKODRAN Mustafi amebainisha kwamba, hajui majaliwa yake ya baadaye kama ataendelea kuichezea Arsenal.

Mchezaji huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 27, ameonekana kuimarika katika miezi ya hivi karibuni akiwa chini ya kocha Mikel Arteta, lakini kusimama kwa ligi za Ulaya kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19) kumemwathiri.

Na licha ya beki huyo kumsifia Arteta kwamba amembadilisha kwa staili yake ya uchezaji, lakini haoni kama ataendelea kuwapo hapo kwenye dimba la Emirates.

"Nimecheza mara kwa mara chini ya Mikel Arteta, pia kwenye Ligi Kuu. Hilo kwa uhakika kabisa limenisaidia na najisikia vizuri.

"Naelewa staili yake ya soka, na namna anavyotaka mimi nicheze, hilo linanifanya nijisikie vizuri zaidi.

"Kwa uhakika amenisaidia, lakini sijui nini kitatokea, maana sijui kama nitaendelea kucheza hapa au la."

Licha ya Arsenal kuonyesha mabadiliko baada ya ujio wa Arteta Desemba mwaka jana, lakini bado ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England ikipitwa pointi nane na Chelsea waliopo nafasi ya nne na wanaowinda nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

HABARI MICHEZO

# Pogba njia nyeupe sasa kurudi Juve

**MANCHESTER,** England

JUVENTUS wanaweza kumpeleka Paul Pogba pale Turin, lakini itawagharimu wao kumtoa nyota wao mmoja.

Pogba mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Manchester United, baada ya kurudi pale Old Trafford mwaka 2016.

Lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wanaweza kuwa tayari kumtoa nyota wao kwa ajili ya kumpata nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Na sasa kwa mujibu wa gazeti la Tuttosport, Pogba mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 2018, anaweza kurudi Juventus kwa fedha pamoja na Paulo Dybala au Miralem Pjanic.

Dybala alikaribia kutua pale Old Trafford kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini ameripotiwa kwamba anakaribia kuongeza mkataba wa kuendelea kukaa pale Juventus.

Huku Pjanic ambaye amecheza mechi 32 kwenye mashindano yote msimu huu pale, akiwa ametua hapo kutoka kule AS Roma mwaka 2016, anaonyesha kuwa anataka kuondoka.





# ENRIQUE AMPELEKA INIESTA ANGA ZA MESSI

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa timu ya Taifa ya Hispania, Luis Enrique amebainisha kwamba, Andres Iniesta ni mmoja wa wachezaji aliyekaribiana kipaji na Lionel Messi ambaye amewahi kumnoa.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, Messi anatajwa kama mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote.

Luis Enrique aliwanoa Messi na Iniesta pale Barcelona kuanzia mwaka 2014 hadi 2017.

Katika mahojiano ya maswali na majibu kwenye ukurasa wa facebook wa timu ya Taifa ya Hispania, Enrique aliwazungumzia wote Iniesta, ambaye kwa sasa anacheza soka kule Vissel Kobe, na Messi.

"Mchezaji aliyenivutia zaidi katika kipindi changu cha ukocha pale Barcelona, bila shaka yoyote ni Leo Messi," alisema.

"Halafu naweza kusema Andres Iniesta alikaribia kuwa sawa na Leo Messi.

"Lakini Messi yupo tofauti kabisa kwenye suala la heshima na kwa wengine."

# Bayern Munich yakataa Alaba na Sane kupishana

**MUNICH,** Ujerumani

OFISA Mtendaji wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amesisitiza kwamba, hakuna mpango wowote wa kumhusisha David Alaba kwenye usajili wa Leroy Sane kwani "jambo hilo halina ukweli."

Majaliwa ya wote wawili Alaba pale Bayern na Sane kule Manchester City bado hayajajulikana huku wote mikataba yao ikitarajiwa kumalizika mwaka 2021.

Uvumi wa kutaka kuondoka kwa mchezaji wa kimataifa wa Austria, Alaba mwenye umri wa miaka 27, umepamba moto hasa baada ya kuripotiwa kumchukua wakala mpya, huku Real Madrid, Barcelona na Chelsea zikitajwa kuwa ndiko sehemu anayotaka kwenda.

Sane, ambaye bado hajacheza mchezo wowote wa Ligi Kuu ya England msimu huu kutokana na majeraha ya goti, kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na Bayern na vinara hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, wanaweza kufufua mpango wao huo mara tu dirisha la usajili litakapofunguliwa, ingawa suala la kumhusisha Alaba kwenye usajili huo limepigwa na Rummenigge.

"Kama nilivyosikia, uvumi unasambaa kwamba tutamtoa David Alaba kwenda Manchester City kwa kubadilisha na Leroy Sane," alisema akiiambia TZ.

"Kwa nyongeza, nasema wazi kabisa: Mpango huo hauna ukweli wowote."

Madai kwamba, wakala wa Alaba ndiye anayepanga hilo, Rummenigge aliongeza: "Ningependa kusema kwa uhakika kabisa, hakuna mpango huo kwa Bayern."

Alaba ni mmoja wa wachezaji waliocheza kwa muda mrefu zaidi pale Bayern na mkataba wake unamalizika kipindi kijacho cha majira ya joto.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RASHFORD ATANGAZA FITI KURUDI UWANJANI

● ● ● Asema ni suala tu la kurudi dimbani haraka kuanza mazoezi kwa kucheza mechi kwa ajili ya...

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford amesema kwamba anajihisi "kuwa bora zaidi" kuliko mwezi uliopita na anakaribia kurudi kuwa fiti zaidi.

**Rashford amekuwa nje ya dimba tangu katikati ya Januari kutokana na kuumia mgongo, huku kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer akisema mapema mwezi huu, kwamba klabu haitamharikisha kurejea dimbani.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England ameonyesha kuendelea vizuri kuimarika kwa afya yake, anatarajia kuanza mazoezi mara tu ligi itakapoendelea tena baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

"Najisikia vizuri sana," alisema Rashford akiiambia Sky Sports. "Natakiwa kufanyiwa vipimo tena kwa siku kadhaa, lakini kwa sasa najisikia vizuri zaidi ikilinganishwa na wiki mbili au tatu zilizopita. "Nahisi vizuri mara 10 zaidi kwa sasa. Kwa upande wangu, sasa ni suala tu la kurudi dimbani haraka kuanza mazoezi kwa kucheza mechi kwa ajili ya timu yangu.

"Nipo vizuri zaidi kwa sasa. Nina furaha zaidi kuliko ilivyokuwa mwezi mmoja uliopita, mambo yanaonekana kuwa safi kabisa."

Rashford ameongeza kusema kwamba, kwa sasa anafanya mazoezi nyumbani kutokana na mlipuko wa virusi vya COVID-19.

"Kila mmoja anajaribu kupambana na hali hii kwa namna anavyoweza," aliongeza kusema.

"Nimekuwa ndani ya nyumba yangu nikifanya mazoezi kwenye gym yangu na naimarika, nasoma vitabu, naangalia muvi na kufanya kile kinachowezekana kufanywa ili muda uende.

"Kwa hakika hakuna kitu chochote unachoweza kufanya kama vile upo kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na kuwa na timu, hivyo najaribu kukabiliana na hali hii.

"Nilitakiwa kuwa nje kwa sababu ya majeruhi, lakini nina bahati kwamba ndani ya gym yangu kuna baiskeli. Hakuna kitu kilichobadilika sana kwangu, kwa sababu bado naweza kufanya mambo yangu ya kila siku ambayo nilikuwa nafanya."

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA FEDERICO

MANCHESTER United inaweza kulipa pauni milioni 450 kwa Real Madrid kama wanataka kumsajili mshambuliaji wake kinda wa miaka 21, Federico Valverde raia wa uruguay. ***(Sunday Mirror)***

### SIMEONE KUKATWA MSHAHARA

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone ndiye kocha anayelipwa zaidi, atatakiwa angalau kukatwa asilimia 30 ya mshahara wake wa pauni milioni 3.3 kwa mwezi. ***(Sunday Times)***

### ARSENAL YAMNYATIA FEKIR

KLABU ya Arsenal inaonekana kufikiria kumsajili Nabil Fekir ambaye walijaribu kumuwania mwaka jana na sasa wanapanga kumchukua kutoka kule Real Betis ya Hispania. ***(Daily Star)***

### MARCELO KUONDOKA MADRID

HUKU majaliwa yake yakiwa hayajajulikana, beki wa Real Madrid, Marcelo anaweza kuondoka klabuni hapo, huku Juventus ikitajwa kumuwania. ***(Marca)***

### EVERTON YAMPA OFA GABRIEL

KLABU ya Everton imetoa ofa ya pauni milioni 30 kwa mchezaji wa kimataifa wa Brazil, Gabriel Magalhae, 22, anayecheza katika klabu ya Lille. ***(Football Insider)***

### SHAQIRI KUUZWA SEVILLA

KLABU ya Liverpool inajiandaa kumuuza winga wa kimataifa wa Uswisi, Xherdan Shaqiri, huku Sevilla ikiwa imeonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Talksport)***

### KLOPP APEWA MASHARTI

MSHAMBULIAJI anayewindwa na kocha Jurgen Klopp, Timo Werner, 24, kutoka RB Leipzig ya Ujerumani atataka kutumia namba ileile ya jezi anayotumia sasa akitua pale Liverpool. ***(Sunday Express)***

### WAKALA AMTETEA COUTINHO

WAKALA wa nyota wa Barcelona, Philippe Coutinho amekanusha madai kwamba, mchezaji huyo amemlalamikia mwenyekiti wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy baada ya dili lake la kuhamia timu hiyo kukwama. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 27, kwa sasa anacheza kwa mkopo pale Bayern Munich. ***(Sunday Star)***

### ROMA YAMUWANIA COSTA

KLABU ya AS Roma inawania kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Atletico Madrid na Chelsea, Diego Costa. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alikaribia kusajiliwa katika klabu hiyo mara mbili hapo kabla. ***(Mundo Deportivo)***

### POGBA, DYBALA KUPISHANA

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba anaweza kurudi Juventus kwa fedha pamoja na Paulo Dybala au Miralem Pjanic kwenda Old Trafford. ***(Tuttosport)***

### VAZQUEZ KUONDOKA REAL

MCHEZAJI Lucas Vazquez anaweza kuondoka Real Madrid kwa sababu hadi sasa hakuna mazungumzo yoyote yaliyofanyika kwa ajili ya kuongeza mkataba wake ambao unamalizika mwakani. ***(AS)***

HABARI MICHEZO

# Kikwajuni yabadili gia angani Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI mwanzoni mwa msimu malengo yao yalikuwa kupanda Ligi Kuu msimu ujao, sasa timu ya Kikwajuni imesema lengo lao ni kubaki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ilipo, baada ya upepo kubadilika.

Aidha, imesema kuburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo haimaanishi kama ndiyo tiketi ya kushuka daraja, bali kama ligi hiyo itaendelea tena kuchezwa wanauhakika watabaki walipo.

Wakongwe hao katika medali ya soka visiwani Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, wapo nafasi ya 13 katika msimamo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja alama 14, huku tayari wakiwa wameshacheza michezo 18 za ligi hiyo ambayo inajumla ya timu 13.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki, Naibu Katibu Mkuu wa timu hiyo, Juma Abdallah, alisema mipango yao kwa sasa ipo katika kulinda daraja na si kutarajia kupanda kutokana na nafasi waliyokuwapo katika msimamo wa ligi hiyo.

Alisema licha ya mipango hiyo ambayo kwa sasa inaonekana migumu kutokana na kusimama shughuli zote za michezo ikiwamo mazoezi, kama watachezaji wataamua kuibakisha katika daraja hilo, ni jambo linalowezekana.

"Awali wakati tunaanza kucheza ligi mipango yetu ilikuwa ni kuhakikisha tunacheza Ligi Kuu msimu ujao, lakini kwa sasa hatuzungumzii tena kupanda daraja bali tunachoangalia ni kuweza kulinda daraja hili tulilopo, kama tunavyojua ligi daraja la kwanza ndio ngumu kuliko zote kutokana na kila timu inawania kupanda," alisema.

# Kaseba atoa somo ubora 'Kickboxing'

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa mchezo wa ngumi na mateke 'Kickboxing', Japhet Kaseba amesema wakati huu ambao michezo imesimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), anakitumia vema katika kujifua ili kujiweka fiti tayari kurejea ulingoni baada ya mapumziko ya mwezi mmoja yaliyotangazwa na serikali.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kaseba aliwataka mabondia wenzake waendelee kufanya mazoezi na wasibweteke na mapumziko haya ya mwezi mmoja.

"Mimi naendelea na mazoezi binafsi ili kuinua zaidi kipaji changu, najua bila mazoezi sitimizi lengo langu," alisema Kaseba na kuongeza, kuwa kipindi kilichopita wengi walikuwa wanauogopa mchezo huo, lakini kwa sasa mwamko umekuwa mkubwa.

Aidha, alisema anaungana na kauli ya serikali ya kutofanyika mashindano mpaka hapo tarehe iliyopangwa ifike kwa kuwa virusi hivyo vimekuwa janga la kimataifa na tayari vimesababisha maelfu ya watu duniani kupoteza maisha.

# MWAMNYETO KUONDOA MABEKI WAWILI SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ikielezwa tayari Simba imemalizana na beki kisiki wa Coastal Union ya Tanga, Bakari Mwamnyeto, taarifa zimeibuka kuwa ujio wake utapukutisha mabeki wawili ndani ya kikosi hicho cha mabingwa wa Ligi Kuu Bara.

**Mwamnyeto amekuwa katika kiwango cha juu sana msimu huu huku akipata namba kwenye kikosi cha kwanza cha timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars iliyoko chini ya kocha Mrundi Etienne Ndayiragije.**

Tayari uongozi wa Simba upo katika mchakato wa kuisuka upya timu hiyo ikiwa ni pamoja na kupukutisha baadhi ya wachezaji walionekana kukosa namba katika kikosi cha kwanza kuelekea msimu wa 2020/21.

Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mazingiza amesema hawataki kufanya makosa katika usajili na kwamba mpango wao ni kuongeza nyota wasiopungua wawili kutoka ndani na wengine tayari maskauti wa klabu hiyo wapo kazini kumulika kwingineko Afrika.

Licha ya mtendaji huyo kutokuwa tayari kutaja moja kwa moja wachezaji watakaotemwa, ila ni wazi beki Paul Bukaba anayekipiga kwa mkopo Namungo FC hatarejeshwa tena kutokana na kiwango chake kuelezwa na mmoja wa viongozi wa Simba kutolivutia benchi la ufundi la timu hiyo lililopo chani ya Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

Lakini Yusuph Mlipili ambaye tangu Sven atue kurithi mikoba ya Mbelgiji mwenzake, Patrick Aussems, hajampa nafasi ya kucheza, naye ni miongoni mwa watakaofunguliwa mlango wa kutokea kwa mujibu wa chanzo chetu ndani ya benchi la ufundi.

"Malengo ya Simba ni kutoa ushindani mkubwa kwenye mechi za kimataifa [Ligi ya Mabingwa Afrika], hivyo wachezaji ambao hawajapata nafasi ya kucheza msimu huu, watakuwa wa kwanza kufunguliwa mlango wa kutokea kipindi cha usajili.

"Klabu inataka kuimarisha timu kwa kusajili nyota wa kiwango cha juu watakaotoa ushindani kwa wanaopata nafasi kikosi cha kwanza, hivyo wale wa benchi hawatakuwa na nafasi," kilieleza chanzo chetu ambacho kilikiri pia Mwamnyeto ameshamalizana na miamba hiyo ya Msimbazi jijini Dar es Salaam.

Wakati huu Ligi Kuu Bara ikiwa imesimama kuepuka kasi ya maambukizi ya virusi vya corona, Simba ipo kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi 71, hivyo ina nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa na kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.



Mshambuliaji wa timu ya Mtibwa Sugar ya Morogoro, Stahmil Mbonde akiwa katika nyuso za furaha na mkewe baada ya kufunga ndoa Jumamosi iliyopita jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *KMC yaahidi kasi mpya corona ikipita*

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya KMC FC imeahidi kurudi kivingine pindi Ligi Kuu itakapoanza baada ya serikali kuisimamisha kwa mwezi mmoja kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa KMC, Haruna Hererimana, alisema atarudi na kasi mpya ili kuhakikisha timu hiyo inashika nafasi nzuri na kukwepa janga la kushuka daraja.

"Nikirudi nitahakikisha napambana timu yangu ishike nafasi nzuri katika msimamo wa Ligi Kuu," alisema Hererimana.

Kocha huyo alisema wakati Ligi Kuu inasimama timu yake ilikuwa imeanza kukaa katika mstari baada ya kupata pointi tatu katika mechi tatu mfululizo.

"Niliwapa wachezaji wote programu za kuendelea nazo ili kuiweka sawa miili yao katika kipindi chote cha mapumziko, hivyo ninaamini watatekeleza na tukirejea mambo yataendelea kuwa sasa," alisema.

Aidha, alisema mlipuko wa corona umempa changamoto kutokana na kwamba tayari alijipanga kwa michezo iliyokuwa mbele yao.

Aliwasisitiza wachezaji wake kufanya juhudi ya kufanya mazoezi binafsi ili Ligi Kuu ikianza wasiwe wazito.

"Nasisitiza kila mchezaji wangu afanye mazoezi kwa umakini mkubwa kwa sababu ukikaa bila mazoezi unaharibu kila kitu," alisema kocha huyo ambaye hadi ligi hiyo inasimama timu yake ipo nafasi ya 15 ikiwa na alama 33 baada ya kushuka dimbani mara 29.

Michezo
Jumatatu Machi 30, 2020
Nipashe



Rashford atangaza fiti kurudi uwanjani UKURASA 30

MAWINDONI...




Mshambuliaji wa Namungo FC, Reliants Lusajo (kushoto), anayewindwa na Yanga, akitoa upinzani dhidi ya wachezaji wa Azam FC wakati timu hizo zilipokutana msimu huu. **PICHA: MAKTABA**

## Iniesta apelekwa anga za Messi

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa timu ya Taifa ya Hispania, Luis Enrique amebainisha kwamba, Andres Iniesta ni mmoja wa wachezaji aliyekaribiana kipaji...




HABARI UK. 29

## Wanaowania tuzo Mchezaji Bora EPL

**LONDON,** England

LIGI Kuu nyingi duniani kwa sasa zimesimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19) na moja ya waathirika wakubwa...



HABARI UK. 20

# Eymael amtaja Lusajo Yanga

## Namungo FC yakiri kufahamu mpango huo, yahaha kumshawishi abaki, lakini mambo yaelekea...

**Na Saada Akida**

HUKU wakihaha kuwaongezea wachezaji wao wa zamani mikataba mipya, uongozi wa Klabu ya Yanga umeweka wazi juu ya ripoti waliokabidhiwa na Kocha Mkuu, Mbelgiji Luc Eymael kwamba imependekeza wachezaji kadhaa wanaocheza Ligi Kuu Bara, akiwamo kiungo mshambuliaji wa Namungo FC, Reliants Lusajo.

**Taarifa za uhakika zilizolifikia Nipashe jijini Dar es Salaam jana kutoka ndani ya Kamati ya Utendaji Yanga imeeleza kuwa Eymael amependekeza kusajili washambuliaji wawili namba tisa na 10.**

Mjumbe mmoja wa kamati hiyo ya utendaji, ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, alisema kati ya washambuliaji ambao Eymael ameeleza kuwahitaji katika ripoti yake kuelekea msimu ujao ni Lusajo.

"Malengo yetu ni kutimiza mahitaji ya timu yetu, hasa kusajili kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi, kweli Lusajo ni miongoni mwa waliopendekezwa katika ripoti ya Eymael," alisema.

Alisema hawataenda kinyume cha mapendekezo ya ripoti hiyo waliyopewa na kwamba watahakikisha wanafuata vyote vilivyoelezwa hatua kwa hatua.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu, alipoulizwa kuhusu mpango huo wa Yanga, alisema wanafanya juhudi za kumbakiza nyota huyo ndani ya timu yao kwa msimu ujao.

Alisema mkataba wa Lusajo unamalizika mwishoni mwa msimu huu, hivyo tayari wameanza mazungumzo na nyota huyo kwa lengo la kuendelea kuipata huduma yake msimu ujao.

"Tumepata taarifa kwamba Yanga wanamhitaji Lusajo, na sisi tumeanza mazungumzo naye ila hatuwezi kumzuia kwenda Yanga inategemea na wenzetu kama watapanda dau zaidi yetu," alisema Zidadu.

Alisema licha ya kwamba Yanga ni timu kubwa, ila hawatakuwa wanyonge kwa kukubali kumwachia kirahisi kwa kuwa watafanya juhudi zote kumbakiza.

Mbali na Lusajo, ambaye ni usajili mpya, Yanga tayari imefanikiwa kumbakisha nyota wao, Mghana Bernard Morrison kwa kumsainisha mkataba wa miaka miwili, hivyo kumzuia kutua kwa watani wao, Simba walikuwa wakimnyemelea.

Hata hivyo, bado haijafahamika endapo imefanikiwa kumalizana na Kiungo Mkabaji, Papy Tshishimbi ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu na amekuwa katika rada za Simba.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >